ISSN 2961 - 6255

# USAFIRI ARDHINI

TOLEO LA SABA

Aprili - Juni 2025



## MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA, LATRA YAJIVUNIA KUKUZA MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA Uk. 01

## UWAMWA RASMI WAKALA WA LATRA

**Bw. Elikana Balandya, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza amekabidhi Cheti cha Uwakala wa kutoa leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa Ushirika wa Wasafirishaji Mkoa** ................. Uk. 07




tiketi.latra.go.tz

pis.latra.go.tz

0681 300 800 Tuma ujumbe WhatsApp

# TAHARIRI

Msomaji wa Jarida la USAFIRI ARDHINI, hili ni toleo la saba linalojumuisha habari na matukio yaliyorindima kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2025. Katika jarida hili, utafahamu jitihada mbalimbali za Serikali zinazotekelezwa na Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ili kuboresha sekta ya usafiri ardhini nchini.



Katika kipindi hiki, tumefanikiwa kudhibiti sekta ya Usafiri wa Barabara, Usafiri wa Reli na Usafiri wa Waya kwa weledi na ufanisi ili kutimiza maono ya Serikali ya kuwa na usafiri ardhini wenye manufaa kwa Serikali, Wasafirishaji na Wananchi. Haya yote utayafahamu kwa kina kwenye jarida hili kupitia makala ya mafanikio ya LATRA ndani ya Miaka Minne ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile, tunajivunia kuendelea kubuni na kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayosaidia utendaji kazi wa Mamlaka na utoaji wa huduma kwa wadau wetu. Mathalan, kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ambapo kufikia Machi, 2025, umeunganisha mabasi yote ya masafa marefu ambayo ni 11,826 yaliyopewa leseni na kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa treni za Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi alizungumza kwa kina Bungeni alipowasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2025/26 na taarifa kamili utaisoma ndani ya jarida hili.

Pia, tumewakumbusha watoa huduma wa Tiketi Mtandao wasio unganisha mifumo yao na Mfumo wa Safari Tiketi wa LATRA na Mfumo wa TRA EFDMS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukamilisha matakwa ya usajili kwa mujibu wa Sheria kabla ya tarehe 1 Julai 2025. Mamlaka inafanya hivi ili kuimarisha usimamizi na kuhakikisha Serikali inapata mapato yatakayowezesha kutekeleza miradi mbalimbali nchini.

Sambamba na hayo, tumeendelea kutoa elimu kwa Madereva na Wamiliki wa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu ili waweze kujiunga na kuunda vyama vya ushirika ambavyo vitawaunganisha na vitawasaidia kuinuana kiuchumi na kijamii. Tumefanikiwa kutoa elimu hiyo kwa walengwa Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Kasulu Mkoa wa Kigoma pamoja na mikoa mingine nchini. Mamlaka tunatoa asilimia 20 ya mapato kama gawio watakalolitumia kulingana na malengo waliyojiwekea.

Hayo ni machache kati ya mengi utakayosoma na kujifunza ndani ya jarida hili. Mamlaka itaendelea kusimamia sekta inazozidhibiti kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha wadau wote wa usafiri ardhini wananufaika na sekta yao. Kwa maoni yoyote, usisite kuwasiliana nasi kwa namba zetu bila malipo 0800110019 / 0800110020 au kupitia Mfumo wa e -mrejesho unaopatikana kwa anwani https://emrejesho.go.tz/ au kwa kufika ofisi ya LATRA iliyo karibu yako. Pia, tutumie ushahidi wa video na picha zinazohusu uvunjifu wa Sheria za Usafiri Ardhini kwa namba ya WhatsApp 0681300800, nasi tutazifanyia kazi kwa wakati.

Nikutakie usomaji mwema wa jarida hili

***"Pamoja kwa Usafiri Bora"***

.........................................

**CPA Habibu J. S. Suluo**

# MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA, LATRA YAJIVUNIA KUKUZA MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akielezea mafanikio ya LATRA katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.*

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, LATRA inajivunia kubuni na kukuza matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye utoaji wa huduma za usafiri ardhini nchini. CPA Suluo amebainisha hayo kwenye mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.

CPA Suluo ameitaja mifumo iliyobuniwa na inayotumiwa na LATRA kuwa ni Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Reli na Barabara (Railway and Road Information Management System - RRIMS), Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App), Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaofahamika kwa jina la Safari Tiketi, Mfumo Shirikishi wa Huduma kwa Wateja pamoja na Mfumo wa e-Mrejesho.

"Mfumo wa RRIMS unawezesha utoaji leseni, usajili wa madereva, malipo na taarifa za udhibiti uliounganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA ili kurahisisha uhakiki wa taarifa za mteja. Pia, unamwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 bila uhitaji wa kufika ofisi za LATRA, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa usumbufu na muda wa kupata huduma," ameeleza CPA Suluo.

Kwa upande wa Mfumo wa VTS, CPA Suluo amesema kuwa ni mfumo unaosimamia usalama wa huduma unaotumia 'Satellite', Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), Mtandao wa Mawasiliano na Vifaa vya Uhifadhi Data Taarifa (GPS Data Servers) vinavyofanya kazi kwa pamoja ili kutuma taarifa za mwenendo wa safari za chombo husika.

"Kufikia Machi 2025, jumla ya magari 11,826 yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo ambapo kati ya hayo, magari 8,969 yanayotuma taarifa kwenye mfumo mpaka sasa. Katika magari yasiyotuma taarifa, baadhi hayapo barabarani kutokana na sababu mbalimbali kama vile Matengenezo ya muda mrefu, ajali, kuungua moto na baadhi yamebadili njia na kuhamia kwenye njia ambazo hazina uhitaji wa kufunga VTS," ameeleza CPA Suluo.

>>>> *Inaendelea Uk. 03*

*<<<< Inatoka Uk. 02*

Pia, ameutaja Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App) unaopatikana kwenye simujanja ‘Play Store’ za aina ya Android, unamuwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi, kutambua uhalali wa leseni za magari na adhabu, hivyo kumuwezesha abiria kuepuka kutumia gari lenye changamoto ili kujiepusha na usumbufu.

CPA Suluo amesema LATRA kwa kushirikiana na wadau wametengenza Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) au Safari Tiketi uliounganishwa na mifumo mingine ya utoaji tiketi ukiwemo wa TRC na mifumo ya tiketi za mabasi ili kurahisisha ukataji tiketi na kutunza taarifa za abiria ambapo ukikamilika utaelekezwa kwenye mabasi ya mijini (daladala) na usafiri wa kukodi.

“Tangu kuanza kuunganisha mifumo ya Tiketi za Kielektroni kwenye CeTS, tarehe 02/08/2024 hadi tarehe 31/03/2025, taarifa zetu zinaonesha jumla ya abiria (miamala ya tiketi za kielektroniki) 13,429,549 ilifanyika kwenye CeTS. Idadi hii ni sawa na wastani wa abiria (miamala) 58,137 zinaonekana kwa siku, sawa na wastani wa abiria (miamala) 1,744,100 kwa mwezi katika kipindi hicho cha siku 231, takriban miezi nane tangu kuanza kutumia mfumo huu,” amefafanua CPA Suluo.

Vilevile amesema LATRA inapokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi na kuyashughulikia kutumia Mfumo Jumuishi wa Huduma kwa Wateja ambapo mwananchi anaweza kupiga simu bila malipo kwa namba 0800110019 au 0800110020 na pamoja na Mfumo wa Kutuma, Kupokea na Kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi (e-Mrejesho) unaopatikana kwa anwani https://emrejesho.gov.go.tz/ kwa kupakua mfumo tumizi wa e-Mrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya LATRA www.latra.go.tz sehemu ya tovuti mashuhuri.



# LATRA YAENDELEA KUIMARISHA USAFIRI ARDHINI KUPITIA TEHAMA



*Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akiwasilisha Bungeni Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa Fedha 2025/26 Mei 16, 2025*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kuimarisha utendaji kazi, utoaji wa huduma bora pamoja na usalama wa sekta ya usafiri ardhini kupitia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa katika shughuli za kidhibiti.

Akiwasilisha Bungeni Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2025/26, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi amesema hadi kufikia Machi, 2025, Mamlaka imeunganisha mabasi yote ya masafa marefu ambayo ni 11,826 yaliyopewa leseni kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa treni za Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

"Mfumo unaonesha kuwa, wastani wa mabasi 8,969 yanatuma taarifa kila siku, sawa na asilimia 76 ya mabasi yote. Aidha, mabasi 2,857 yaliyobaki ambayo ni asilimia 24 ni mabasi yaliyosimama kutoa huduma kwa sababu mbalimbali zikiwemo ajali na matengenezo,"amesema Mhe. Prof. Mbarawa.

Vilevile amesema, ili kuongeza wigo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi, LATRA imewezesha upatikanaji wa taarifa za mabasi kupitia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa anwani pis.latra.go.tz/ uliounganishwa na VTS unaowasaidia abiria na wadau wa usafiri nchini kufahamu taarifa za mabasi yanayoelekea vituo vya mabasi vilivyo karibu yao na kuwawezesha wadau hao kufahamu mwendokasi na mahala lilipo basi husika.

Wakati huohuo Mhe. Prof. Mbarawa (Mb) ameeleza kuwa LATRA inaendelea na mchakato wa kujenga dirisha moja la utoaji wa huduma za tiketi za abiria kwa wasafiri wa mabasi ya masafa marefu na wasafiri wa treni za reli ya kisasa (SGR) na reli ya kati (MGR) na kwa sasa dirisha hilo lipo katika hatua za mwisho za kuanza kufanya kazi.

"Hadi sasa mfumo huu kwa upande wa treni unafanya kazi kwa ukamilifu na kwa upande wa mabasi utakamilika mara tu

baada ya kukamilika usajili wa mifumo iliyokidhi vigezo vya kuendelea kutoa huduma ya tiketi mtandao ambapo jumla ya mifumo 14 ya watoa huduma imeunganishwa kwenye Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao, kazi hii ya kuunganisha mifumo inatarajiwa kukamilika

**>>>> *Inaendelea Uk. 05***

*<<<< Inatoka Uk. 05*

na kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2025," ameeleza Mhe. Prof. Mbarawa.

Amebainisha kuwa, LATRA imeendelea kutekeleza jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara kupitia mifumo ya TEHAMA.

"Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya madereva 7,232 walisajiliwa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) na kutahiniwa kupitia Mfumo wa Kutahini Madereva (DTS) ambapo kati ya hao madereva 1,550 walithibitishwa na kupatiwa Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i-Button), na Kwa upande wa usajili wa wahudumu hadi kufikia Machi 2025, LATRA ilisajili wahudumu 560 baada ya kupewa mafunzo ambayo yalitolewa kwa kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Elimuya Biashara (CBE)," amefafanua Mhe. Prof. Mbarawa.

Kwa upande wa udhibiti usafiri wa waya, Mhe. Prof. Mbarawa amesema Julai 2024 hadi Machi 2025, LATRA ilishirikiana na wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kutambua uwepo wa fursa, utayari na mahitaji ya udhibiti wa huduma hiyo nchini ambapo wadau kutoka ndani na nje ya nchi 16 wameonesha utayari wa kuwekeza katika usafiri kwa njia ya waya.

"Kutokana na fursa hiyo, Wizara ya Uchukuzi inaandaa Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya baada ya kupokea maoni ya wadau mwezi Desemba 2024 pamoja na kufanya maombi ya mabadiliko ya muundo wa LATRA ili kuwe na kitengo mahsusi katika udhibiti wa usafiri huo" ameeleza Mhe. Prof. Mbarawa.

Mamlaka inaendelea kutekeleza kwa vitendo maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye anasisitiza matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.



# UWAMWA RASMI WAKALA WA LATRA



*Bw. Elikana Balandya, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza amekabidhi Cheti cha Uwakala wa kutoa leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri ardhini (LATRA) kwa Ushirika wa Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza (UWAMWA) Juni 24, 2025, ukumbi wa mikutano wa Mahatma Gandhi, Mwanza.*

Bw. Elikana Balandya, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza amekabidhi Cheti cha Uwakala wa kutoa leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri ardhini (LATRA) kwa Ushirika wa Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza (UWAMWA) Juni 24, 2025, ukumbi wa mikutano wa Mahatma Gandhi, Mwanza.

Akikabidhi Cheti hicho kwa niaba ya Mhe. Said Mohamed Mtanda Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Bw. Balandya amewapongeza wanachama wa UWAMWA kwa hatua hiyo kubwa waliyofikia na amewataka kujisimamia na kuhakikisha wasafirishaji hao wanakuwa na leseni za LATRA na pia amewasihi kutumia vizuri asilimia 20 ya gawio watakalolipata kutokana na leseni watakazozikata ili kuwaletea maendeleo.

Vilevile amewaeleza wasafirishaji hao kuwa, Serikali inahamasisha kuundwa kwa vyama vya ushirika vya watoa huduma za usafiri kama mkakati madhubuti wa kuwawezesha wadau kushirikiana, kupata mikopo kwa urahisi, kuongeza nguvu ya sauti yao katika maamuzi, kuwawezesha kutoa huduma kwa ufanisi na kuzingatia uweledi na kurahisisha uratibu wa shughuli zao.

Wakati huohuo Bw. Balandya amezindua rasmi magari maalumu ya UWAMWA yatakayokuwa yanawachukua wanafunzi wa shule za umma asubuhi na jioni ambapo wazazi watatakiwa kuweka nauli za wanafunzi hao kwenye kadi itakayotumika wakati wote wa kuwasafirisha wanafunzi hao.

Akizungumza kwa niaba ya CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara amesema Cheti hicho kitaruhusu UWAMWA kutoa aina sita za leseni za vyombo vya moto vya kukodi ambazo ni leseni za Pikipiki za Magurudumu Mawili, Leseni za Pikipiki za Magurudumu Matatu, Leseni za Taksi za kawaida, Leseni za Taksi Mtandao, Leseni za Magari Maalumu ya Kukodi pamoja na Leseni za Kuitisha Mtandaoni Usafiri wa Kuchangia

"Sisi kama Mamlaka tunataka kuondoka kwenye utaratibu wa kudhibiti mtu mmoja mmoja na kwenda kwenye mfumo wa udhibiti kupitia vyama vya ushirika au kampuni ambapo wasafirishaji watainuana kiuchumi lakini pia watakuwa wanasimamiana kuhakikisha wanatekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria na utaratibu uliopo huku wakizingatia masharti ya leseni za usafirishaji walizonazo," ameeleza DCP Kahatano.

Naye Bw. Jabir John Magele Mwenyekiti wa UWAMWA amesema anaishukuru LATRA kwa kuwapatia cheti cha uwakala wa utoaji wa leseni za LATRA kwa vyombo vya moto vya kukodi kibiashara kwani cheti hicho kinaashiria urasmi wa UWAMWA kama wakala wa LATRA.

**>>>> *Inaendelea Uk. 07***

<<<< Inatoka Uk. 06



*Wanachama wa UWAMWA wakiwa kwenye picha ya pamoja na mgeni rasmi katika makabidhiano ya cheti cha uwakala kwa chama cha Usirika cha Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza Juni 24, 2025 ukumbi wa mikutano wa Mahatma Gandhi, Mwanza.*

"Naishukuru LATRA kwa kutupatia cheti cha uwakala, cheti hiki kinaenda kuwa chachu ya utendaji kazi wetu ambao matunda yake ni kutuinua kiuchumi kupitia gawio la 20% tutakayorejeshewa na LATRA kutokana na leseni tutakazozikata kwa wanachama wetu," ameeleza Bw. Magele.

Akizungumzia mabasi ya kuchukua wanafunzi wa shule za umma, Bw. Magele ameeleza kuwa, wao kama UWAMWA wameanza na magari 10 kwa sasa yatakayotoa huduma hiyo ikiwa ni sehemu ya mchango wao katika kutatua changamoto za usafiri kwa wanafunzi mkoani Mwanza.

Makabidhiano ya cheti hicho yamefanyika wakati wa Mkutano wa Wadau wa Usafirishaji ulioandaliwa na LATRA na kuhudhuriwa UWAMWA, Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA), Muwakilishi wa Umoja wa Wasafirishaji Jiji la Arusha (UWADAJA) pamoja na wadau wengine wa usafirishaji Mkoa wa Mwanza ambapo walizungumza masuala mbalimbali kwa mustakabali mzuri wa umoja wao na ustawi wa sekta ya usafiri ardhini mkoani hapo na nchini kwa jumla.



*Wadau wa usafirishaji wakiwa kwenye makabidhiano ya cheti cha uwakala kwa chama cha Ushirika cha Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza Juni 24, 2025 ukumbi wa mikutano wa Mahatma Gandhi, Mwanza*

# MHE. SIMBACHAWENE AIPONGEZA LATRA KWA UTENDAJI KAZI NA UBUNIFU WA MFUMO WA PIS




*Mhe. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, akikabidhiwa zawadi na Bi. Rukia Kibwana, Afisa Leseni na Usajili LATRA Dodoma alipotembelea banda la LATRA kwenye maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika viwanja vya Chinangali Park, Jijini Dodoma Juni 16, 2025.*

Mhe. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, amekoshwa na mfumo wa taarifa kwa abiria (PIS), ambao ni mfumo unaomuwezesha abiria kujua basi lilipo, muda wa kuwasili kituoni na kukagua mwendokasi wa basi alilopanda

Mhe. Simbachawene ameyasema hayo Juni 16, 2025 alipotembelea banda la LATRA na kupatiwa elimu ya jinsi mfumo huo unavyofanya kazi kwenye maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.

Vilevile Mhe. Simbachawene amesisitiza wadau kutumia mfumo huo wa PIS kwa kuwa itaondoa udanganyifu kwa abiria wanaosafiri kwa njia ya basi, ambapo wataweza kuona mahali basi lilipo na mwendokasi wa basi husika kwa kutumia simu kiganjani.

Akitoa elimu ya mifumo ya kidigitali inayotumiwa na LATRA, Bi. Rukia Kibwana, Afisa Leseni na Usajili LATRA, amesema kuwa, Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) umeleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya usafiri ardhini kwa kumuwezesha abiria kuona namna mabasi yanavyoingia na kutoka pamoja na kujua mwendokasi wa basi husika.

"Mfumo wa Taarifa kwa abiria (PIS) umetokana na mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS) na tangu kuzinduliwa kwake Julai 2024, mfumo huu umeleta mabadiliko makubwa kidigitali haswa kwenye sekta ya Usafiri Ardhini kwa kuwezesha abiria kuwa na ratiba ya magari yote yanayotoka na kuingia nchini, pamoja na mwendokasi wa basi husika na mpaka sasa umefungwa kwenye stendi kuu mbili ya Magufuli mkoani Dar es salaam na Nanenane jijini Dodoma", amesema Bi. Rukia.

Pia Bi. Kibwana aliongeza kuwa mbali na mfumo wa PIS kuna mfumo wa Uthibitishaji wa Madereva (DTS) kuwa ni mfumo wa kielektroniki wa kutahini madereva, ambapo dereva anatakiwa kujisajili kwa kutumia namba yake ya NIDA kwenye mfumo mama wa usimamizi wa taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) na kuweka nafasi ya kufanya mtihani na kisha kuchagua tarehe na muda atakapoenda kufanya mtihani.

LATRA inatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika jijini Dodoma, inayosema Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidigiti ili kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji, ambapo kupitia maadhimisho hayo, LATRA inatoa elimu ya mifumo mbalimbali ya kidigitali inayotumiwa na Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake.

# MHE. KIHENZILE AKOSHWA NA UBUNIFU WA MIFUMO YA LATRA



*Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi akitoa pongezi kwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) baada ya kupatiwa elimu kuhusu mifumo inayotumiwa na LATRA katika shughuli za udhibiti alipotembelea banda la LATRA kwenye Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma Juni 19, 2025.*

Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri - Uchukuzi ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa utendaji kazi na ubunifu wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imerahisisha utoaji wa huduma kwa wadau.

Mhe. Kihenzile ametoa pongezi hizo Juni 19, 2025 alipotembelea banda la LATRA kwenye Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

“Nawapongeza sana LATRA kwa kuendelea kuwa wabunifu wa mifumo mbalimbali ambayo mnaitumia kurahisisha huduma za usafirishaji nchini mfumo wa kwanza ni mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS) ambao wananchi wameupokea vizuri sana kwa kuweza kuona chombo kipo wapi na kinatembea kwa mwendokasi gani na tunategemea kufanya tathmini baada ya mwaka mmoja kujua kama ajali za barabarani zimepungua” amesema Mhe. Kihenzile.

Naye, Bw. Ezekiel Emmanuel, Afisa Mfawidhi LATRA Dodoma, alimueleza Mhe. Kihenzile kuwa, Mamlaka inatekeleza kwa vitendo maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kubuni na kutumia Mifumo ya TEHAMA inayoongeza tija ya utendaji kazi na usimamizi wa huduma.

Vilevile Bw. Emmanuel amesema kuwa, ili kuongeza tija ya udhibiti wa sekta ya usafiri ardhini pamoja na kuongeza wigo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi, LATRA imewezesha upatikanaji wa taarifa za mabasi kupitia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa anwani pis.latra.go.tz/ uliounganishwa na mfumo mama wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ambao umeleta manufaa makubwa kwakuwa umechangia sana kubadilisha tabia za madereva wanapokuwa barabarani na chombo cha moto.

“LATRA inagusa abiria na watoa huduma wa kawaida kabisa na tumeweza kuboresha huduma kwa kuanzisha mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaomuwezesha abiria kujua mahali basi lilipo na mwendokasi wa basi, mfumo huo umetokana na mfumo mama wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaoweza kudhibiti mwendokasi wa mabasi ya masafa marefu, amefafanua Bw. Emmanuel.

**>>>> *Inaendelea Uk. 10***

**<<<< Inatoka Uk. 09**

Ameongeza kuwa LATRA kwa sasa imerahisisha huduma za utoaji wa leseni ambapo mtoa huduma anaweza akaomba leseni bila kuwa na haja ya kufika ofisini kwa kuingia tu kwenye mfumo wa Usimamizi wa Reli na Barabara (RRIMS) kwa anwani rrims.latra.go.tz na kufanya maombi ya leseni na kupata namba ya kumbukumbu ya Malipo popote pale alipo na akisha lipia anaweza kuchapa leseni yake.

Aidha, Bw. Emmanuel ameitaja mifumo mingine inayotumiwa na LATRA ni Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App), Safari tiketi, mfumo wa Uthibitishaji wa Madereva (DTS) pamoja Mfumo wa Taarifa kwa abiria (PIS).

LATRA inashiriki kwenye maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma jijini Dodoma kuanzia Juni 16 hadi 23, 2025 ambapo wadau wa sekta ya usafiri ardhini wanapatiwa elimu kuhusu mifumo mbalimbali inayotumiwa na Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake kwa ubora na ufanisi.




***Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA (wa pili kulia) akiwa pamoja na mafisa kutoka LATRA kwenye Maonesho ya wiki ya Mazingira Juni 3, 2025 viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.***

# WATOA HUDUMA ZA TIKETI MTANDAO WASIOSAJILIWA MARUFUKU JULAI 01, 2025



*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano (LATRA) akifanya ukaguzi wa utekelezaji wa masharti ya leseni za usafirishaji abiria uliofanyika Stendi ya Mabasi Msamvu iliyopo mjini Morogoro Juni 14, 2025.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesema ifikapo Julai 01, 2025 watoa huduma wa Tiketi Mtandao wasiounganisha mifumo yao na Mfumo wa Safari Tiketi wa LATRA na Mfumo wa TRA EFDMS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hawatoruhusiwa kuendelea kutoa huduma hiyo.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano (LATRA) wakati wa ukaguzi wa kawaida wa utekelezaji wa masharti ya leseni za usafirishaji abiria uliofanyika Stendi ya Mabasi Msamvu iliyopo mjini Morogoro, Juni 14, 2025.

Bw. Pazzy amesema kuwa, hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha usimamizi wa sekta ya usafiri ardhini, kuongeza uwazi katika ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha abiria wanapata huduma kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zilizopo.

"Hadi sasa watoa huduma wachache kati ya 15 wamekamilisha usajili na kuunganisha mifumo yao na mifumo ya Serikali na Julai 01, 2025 tutatoa orodha ya watoa huduma walioidhinishwa na Serikali ili wafahamike na wasafirishaji na hao ndio watakuwa wanatambulika kutoa huduma hiyo," ameeleza Bw. Pazzy.

Vilevile amesema, kwa mujibu wa Sheria, wasafirishaji wanaruhusiwa kumiliki mifumo yao wenyewe ya mauzo ya tiketi mtandao na pia wanaweza kuchagua watoa huduma wa tiketi mtandao walioidhinishwa na LATRA ambao kwa mujibu wa Kanuni za Tiketi Mtandao, wanapaswa kupewa cheti kutoa huduma hiyo.

Aidha, Bw. Pazzy amewataja watoa huduma hao 15 wa Tiketi Mtandao kuwa ni Logix Co Limited, Itule Company Limited, Busbora Company Limited, Duarani Innovate Limited, Web Corporation Tanzania Limited, Hashtech Tanzania Limited, Otapp Agency Company Limited, Sepa Tech Limited, Iyishe Company Limited - Adventure Connection,Global Light & Company Limited, Mkombozi Infotech Company Limited, Meerkatz - Kidia One, Abood Bus Services, Borita Company Limited pamoja na Exabytes Africa Limited.

LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wanaendelea na ukaguzi wa mabasi ya abiria kote nchini unaohusisha ufuatiliaji wa uhalali wa leseni za usafirishaji, matumizi ya mikanda ya usalama, uwekaji wa alama kwenye mizigo ya abiria na uzingatiaji wa matumizi ya Tiketi Mtandao.

# MHE AWESO AIPONGEZA LATRA KWA UTENDAJI KAZI NA UBUNIFU WA MIFUMO




*Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Waziri wa Maji (wa katikati) akipokea zawadi kutoka kwa Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA (kushoto) na Bi. Mambwana Jumbe, Afisa Uhusiano na Mawasiliano LATRA (kulia) alipotembelea banda la LATRA kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira Jijini Dodoma, viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete Juni 2, 2025*

Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Waziri wa Maji ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa utendaji kazi na ubunifu wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imerahisisha utoaji wa huduma kwa wadau.

Mhe. Aweso ametoa pongezi hizo Juni 02, 2025 alipotembelea banda la LATRA kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira yanayofanyika jijini Dodoma, viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete.

Akielezea mifumo hiyo, Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA alimueleza Mhe, Aweso kuwa, Mamlaka inatekeleza kwa vitendo maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kubuni na kutumia Mifumo ya TEHAMA inayoongeza tija ya utendaji kazi na usimamizi wa huduma.

Vilevile Bw. Pazzy amesema kuwa, ili kuongeza tija ya udhibiti wa sekta ya usafiri ardhini pamoja na kuongeza wigo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi, LATRA imewezesha upatikanaji wa taarifa za mabasi kupitia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa anwani pis.latra.go.tz/ uliounganishwa na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaowasaidia abiria na wadau wa usafiri nchini kufahamu taarifa za mabasi yanayoelekea vituo vya mabasi vilivyo karibu yao na kuwawezesha wadau hao kufahamu mwendokasi na mahala lilipo basi husika.

"Kwa sasa msafirishaji hana haja ya kufika ofisini kuchukua leseni yake bali anafuata taratibu zote kuanzia kuomba hadi kuchapa leseni yake yeye mwenyewe kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Reli na Barabara (RRIMS) unaopatikana kwa anwani ya rrims.latra.go.tz/, ameeleza Bw. Pazzy.

Aidha, Bw. Pazzy ameitaja mifumo mingine inayotumiwa na LATRA ni Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App), Mfumo wa Safari Tiketi tiketi.latra.go.tz/ pamoja na Mfumo wa Kutahini Madereva (DTS).

LATRA inashiriki kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira jijini Dodoma kuanzia Juni 01 hadi 05, 2025 ambapo wadau wa sekta ya usafiri ardhini wanapatiwa elimu kuhusu kazi na majukumu ya Mamlaka.

# NW SANGU: ENDELEENI KUTOA ELIMU KWA WANANCHI




***Mhe. Deus Sangu (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akiisihi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuwaongezea uelewa wa majukumu ya Mamlaka alipotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 20, 2025 viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.***

Mhe. Deus Sangu (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ameisihi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuwaongezea uelewa wa majukumu ya Mamlaka.

Mhe. Sangu amebainisha hayo alipotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 20, 2025 viwanja vya Chinangali Park, Dodoma ambapo alielezwa jinsi Mamlaka inavyodhibiti sekta ya usafiri ardhini kwa kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

“Wananchi wanahitaji kuipata elimu hii kwa kina, hivyo ongezeni wigo wa utoaji elimu ili muwafikie wananchi ambao ndio watumiaji wa huduma za usafiri ardhini pamoja na mifumo mnayoendelea kuibuni na kuitumia,” amesema Mhe. Sangu.

Pia, Mhe. Sangu ameipongeza LATRA kwa utendaji kazi mzuri ulioleta mapinduzi makubwa ya uendeshaji na usimamizi wa sekta ya usafiri ardhini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa wakati kupitia mifumo ya TEHAMA.

“Mnafanya kazi nzuri sana, nimeziona kazi zenu na nimebahatika kushuhudia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) katika ofisi zenu pale Mikocheni, Dar es Salaam namna unavyofanya kazi na hakika VTS umesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti ajali nchini,” ameeleza Mhe. Sangu.

Naye Bw. Ezekiel Emmanuel, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dodoma ameeleza namna LATRA inavyorahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) unaopatikana kwa anwani ya rrims.latra.go.tz/

“Kwa sasa msafirishaji anachapa leseni yake popote pale alipo kupitia akaunti yake ya maombi ya leseni ya RRIMS bila yeye kufika katika ofisi za LATRA, na hii inaokoa muda na gharama kwa msafirishaji,” amefafanua Bw.Emmanuel.

Vilevile amebainisha Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) pis.latra.go.tz/ kuwa umerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwakuwa mwananchi sasa anapata taarifa ya safari popote alipo kupitia simu janja yake na mfumo huo umewekwa kwenye runinga za stendi ya mabasi iliyopo nanenane Dodoma na Stendi ya mabasi Magufuli jijini Dar es Salaam.

**>>>> *Inaendelea Uk. 14***

*<<<< Inatoka Uk. 13*

Mamlaka inashiriki vyema kutoa elimu kwa wananchi kuhusu shughuli zake za kiudhibiti katika Maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi kwa Umma yanayofanyika kuanzia Juni 16 hadi 23, 2025 katika viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.







***Mdau wa Usafirishaji akifurahia Mfumo wa PIS baada ya kupata maelezo kutoka kwa Bw. Ezekiel Emmanuel, Afisa Mfawidhi LATRA Dodoma alipotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 19, 2025 viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.***

# ELIMU YA USHIRIKA YAWAFIKIA MAAFISA WASAFIRISHAJI WILAYANI MWANGA, MKOA WA KILIMANJARO




*Wadau wa usafirishaji na baadhi ya Menejimenti na Maafisa wa LATRA wakiwa kwenye mkutano wa kutoa elimu ya umuhimu wa kujiunga katika vyama vya ushirika kwa Madereva na Wamiliki wa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu Wilayani Mwanga Mkoani kilimanjaro, Juni 06, 2025.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kwa kushirikiana na Chama cha Ushirika cha Madereva na Wamiliki wa Bodaboda na Bajaji Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS), Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoani humo, imetoa elimu ya umuhimu wa kujiunga katika vyama vya ushirika kwa Madereva na Wamiliki wa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu Wilayani Mwanga Mkoani kilimanjaro, Juni 06, 2025

Akizungumza katika Mkutano huo, DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA amesema, Mamlaka imelenga kuwawezesha kiuchumi maafisa wasafirishaji wilayani humo kupitia vyama vya ushirika kwani kupitia vyama hivyo Mamlaka itawarejeshea asilimia 20 ya mapato ya leseni za LATRA watakazozikata kupitia ushirika wao hivyo ni muhimu kwa maafisa usafirishaji hao kujiunga na chama cha ushirika.

“Tunataka kutengeneza ajira endelevu kwenu ninyi maafisa wasafirishaji ili mjitegemee kiuchumi, hii ni fursa pana nasi tunapenda iwanufaishe wote na mfahamu tu kuwa Serikali yenu inataka mheshimike kwa kuwa kazi yenu ni sawa na kazi nyingine, pia mtekeleze majukumu yenu kwa kufuata Sheria na Taratibu za usafiri ardhini zilizopo,” ameeleza DCP Kahatano.

Pia, DCP Kahatano amempongeza na kumshukuru Mhe. Joseph Tadayo, Mbunge wa Jimbo la Mwanga ambaye baada ya kuona KIBABOT SACCOS inafanya vizuri Wilayani Moshi, akaona ni fursa ya kipekee kwa maafisa wasafirishaji jimboni kwake kujiunga na SACCOS hiyo ili kubadili maisha yao kiuchumi na kijamii.

Akizungumza na maafisa Usafirishaji, Mhe. Tadayo, Mbunge wa Jimbo la Mwanga amesema Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anataka vijana wawezeshwe ili kujikwamua kiuchumi, hivyo kupitia KIBABOT SACCOS, jambo hilo linaenda kuwanufaisha vijana Wilayani hapo.

“Serikali ipo tayari kuwawezesha lakini kwa utaratibu, hivyo mimi nitawalipia kiingilio ili wote muweze kujiunga na KIBABOT SACCOSS,

**>>>> *Inaendelea Uk. 16***

<<<< Inatoka Uk. 15

hii ni fursa nzuri kwenu ninyi kama vijana na Serikali inawategemea katika ujenzi wa Taifa hili, hivyo kupitia ushirika huu mtakuwa wamoja na kufanya maendeleo kwa pamoja," amesema Mhe. Tadayo.

Naye Bw. Hamad Bendera, Mwenyekiti wa Bodi ya KIBABOT SACCOS amesema kuwa, LATRA iliwapelekea wazo la kuanzisha ushirika, wakalipokea na kulifanyia kazi na hadi sasa ushirika wao umesajiliwa na umeanza kufanya kazi.

"Tulipopata wazo na kuona lina tija, tulijikusanya watu 68 na kwenda kusoma masuala ya ushirika kwenye Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kwa hiyo tunaendesha ushirika wetu kwa ueledi wa hali ya juu. Pia, tumeweza kuajiri wataalam wengine, kwa lengo la kuongeza ufanisi, uwajibikaji na hatimaye tuweze kujisimamia wenyewe ili tufikie malengo tuliyojiwekea ya kuinuana kiuchumi na kijamii," amesema Bw. Bendera.

Vilevile Bw. Bendera amesema KIBABOT SACCOS imedhamiria kufungua tawi lake la kwanza Wilayani Mwanga na hivyo amewasihi maafisa usafirishaji Wilayani humo kujiunga na ushirika huo ili waweze kuboresha maisha yao kwa kuwa kupitia umoja huo, wataweza kukopesheka kirahisi, watakopeshana na pia kufanya uwekezaji kwenye maeneo tofauti ili kujikwamua kiuchumi.

Nao maafisa usafirishaji waliohudhuria mkutano huo, wamesema wamepokea kwa dhati fursa hiyo ya kujiunga na KIBABOT SACCOS na wanaimani kubwa kuwa wanaenda kuboresha hali za maisha yao na familia zao kwa kuwa watanufaika moja kwa moja na ushirika kwa kukopa na kufanya uwekezaji.

Kanuni za LATRA za Usafiri wa Magari ya Kukodi, 2020 ilifanyiwa marekebisho Machi, 2023 na kuruhusu LATRA kukasimu madaraka ya kutoa leseni kwa Wakala aliyethibitishwa ambao ni Vyama Ushirika, Taasisi za Umma (LGA), Kampuni na Watu Binafsi.

Chama cha Kwanza cha Ushirika Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS LTD) ilisajiliwa 3 Agosti 2023. Kwa sasa Wanatoa Leseni za LATRA kwa Pikipiki kutumia Mfumo wa LATRA wa kutoa leseni (RRIMS) na wamepata fursa ya kuaminiwa na Taasisi zingine za umma na kupewa kazi zinazowaingizia mapato, mfano: kusimamia huduma za uegeshaji magari (parking).



# MHE. MPOGOLO AIPA KONGOLE MAUPIDA




*Mhe. Edward Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala (wa tatu kulia) kwenye picha ya pamoja na maafisa usafirishaji kwenye hafla ya kukabidhi cheti cha ushirika kwa Chama cha Ushirika cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (MAUPIDA) Aprili 04, 2025 katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Ilala.*

Mhe. Edward Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala amewapongeza maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda) na pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) kwa kuanzisha Chama cha Ushirika cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (MAUPIDA) kwa kuwa ushirika huo utawawezesha kujikwamua kijamii na kiuchumi ikiwemo kutoka kwenye kuajiriwa mpaka kujiajiri kwa kununua na kumiliki bajaji na bodaboda zao wenyewe.

Mhe. Mpogolo amebainisha hayo wakati akikabidhi cheti cha ushirika kwa chama hicho katika hafla iliyofanyika Aprili 04, 2025 katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Ilala.

"Nawapongeza sana kwa kuanzisha ushirika wenu wa MAUPIDA na hakika ushirika huu utawawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha na pia mtapata gawio la asilimia 20 kutoka LATRA," amesema Mhe. Mpogolo.

Vilevile Mhe. Mpogolo ameihimiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuwapatia uwakala MAUPIDA ili kukusanya mapato kwa niaba ya Mamlaka kwa kuwa zipo pikipiki zaidi ya 150,000 katika halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ndani na pembezoni mwa mji.

Naye Bw. Pateli Ngereza, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, amesema kuwa uanzishwaji wa vyama vya ushirika kwa maafisa usafirishaji umekuwa ni tamanio la Mamlaka na ushirika huo utawezesha watoa huduma wote wa bodaboda na bajaji kupata leseni za LATRA popote walipo kupitia SACCOS yao.

"Hii imekuwa ni kiu yetu ya muda mrefu kuhakikisha kwamba tunawaweka kwa pamoja katika umoja ambao utakuwa na manufaa kwa wanachama, jamii na Serikali kwa jumla na tunaamini kuwa, baada ya kuanzisha SACCOS hii Mamlaka itaingia makubaliano kwa mujibu wa Kanuni za usafirishaji wa kukodi na vyama hivi ambavyo vimeanzishwa kisheria kwa ajili ya kutoa huduma kwa niaba ya Mamlaka. Na hii imekuwa msaada kwetu kuhakikisha kwamba chama hiki kinajisimamia wanasimamiana wenyewe na watoa huduma wote wa bodaboda na bajaji wanapata leseni zetu popote pale walipo kwa SACCOS hii," amefafanua Bw. Ngereza.

Kwa upande wake, Bw. Saidi Kagoma, Mwenyekiti wa ushirika huo ameishukuru Serikali kupitia LATRA kwa jitihada za kuinua hali za maisha ya maafisa wasafirishaji kwa kuwa hamasisha kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika.

**>>>> *Inaendelea Uk. 18***

<<<< Inatoka Uk. 17

“Gharama ya leseni kwa bajaji ni TZS. 22,000/= na bodaboda TZS. 17,000/= na tumeelezwa kuwa tutapata gawio la asilimia 20 na pia tutaweza kukopesheka, hii ni faraja kwetu kwa kuwa tutaweza kuanzisha miradi mbalimbali itakayotuinua kiuchumi na kijamii na pia tunaamini na sisi tutamiliki magari kupitia ushirika wetu,” amesema Bw. Kagoma.

Kwa nyakati tofauti, wanachama wa MAUPIDA wameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuwatambua, kuwajali, kuwalea na kuwathamini, na pia wamefurahi kwa kuwa ushirika wao umepata baraka za Serikali kupitia LATRA na wanaamini hali zao za maisha zinaenda kubadilika kupitia ushirika huo.

## UWADAJA MBIONI KUANZISHA USHIRIKA



***DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) (wa pili kulia) akiongoza kikao kati ya LATRA na wajumbe wa Umoja wa Daladala Jiji la Arusha (UWADAJA) kwa lengo la kufahamu hatua waliofikia ya kuanzisha chama cha ushirika cha wamiliki wa daladala Mkoani humo, Juni 06, 2025.***

DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), amekutana na viongozi na wajumbe wa Umoja wa Daladala Jiji la Arusha (UWADAJA) kwa lengo la kufahamu hatua waliofikia ya kuanzisha chama cha ushirika cha wamiliki wa daladala Mkoani humo, Juni 06, 2025.

Vilevile, DCP Kahatano amewapongeza UWADAJA kwa hatua nzuri waliofikia katika uanzishaji wa ushirika wa chama chao na kuwaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha umoja huo unaoanzisha chama cha ushirika ambacho kitakuwa na msaada kwao wa kiuchumi na kuwawezesha kufungua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa manufaa ya wanachama na ushirika kwa jumla.

“Ushirika mtakaoanzisha utawawezesha kutoa huduma za usafiri kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia ueledi kutokana na nguvu ya kiuchumi katika kumiliki vyombo vikubwa na vya kisasa, kuajiri wataalamu wa fani husika na kuzingatia Sheria katika utoaji huduma,” ameeleza DCP Kahatano.

Kwa upande wake Bw. Alibano Matemwa, Mwenyekiti wa UWADAJA amesema umoja wao ulilenga kujiinua kiuchumi na kijamii, “Ili kutekeleza malengo haya, ilitupasa kufikiria kuwa na taasisi yenye uwezo wa Kisheria hivyo kwa pamoja tukaamua kuanzisha ushirika, maana ni rahisi wa kuendesha pia unatoa nafasi sawa kwa kila mjumbe kushiriki katika kutoa mawazo, maboresho na tunaamini sote tutanufaika na ushirika wetu kwa kufanya mambo makubwa ya maendeleo kwa ajili yetu na familia zetu,” amesema Bw. Matemwa

Kikao hicho kimefanyika katika ofisi ya UWADAJA jijini Arusha na kuhudhuriwa na Bw. Omary Saleh Afisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Arusha pamoja na Wajumbe wa UWADAJA.

# MHE. MUNKUNDA AIPONGEZA LATRA KWA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA



*Mhe. Mwanahamisi Munkunda, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro, akijadili masuala mbalimbali kuhusu sekta ya usafirishaji alipotembelewa ofisini kwake na DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA pamoja na viongozi wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Wamiliki na Madereva wa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOSS) Juni 6, 2025.*

Mhe. Mwanahamisi Munkunda, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kuongeza fursa za ajira kwa maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu kupitia Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS).

Mhe. Munkunda ametoa pongezi hizo Juni 6, 2025 ofisini kwake alipotembelewa na DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA pamoja na viongozi wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Wamiliki na Madereva wa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS).

“Nawapongeza sana kwa jitihada za kutengeneza ajira kwa vijana kwa kuhakikisha wanaunda vyama vya ushirika na kizuri zaidi mnawapatia asilimia 20 ya kamisheni kutoka kwenye ada za leseni zinazopatikana kwa kufanya kazi ya uwakala wa LATRA, jambo hili ni zuri sana na mnatekeleza kwa vitendo maono ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha vijana wanapata ajira, wanainuka kiuchumi na wanaachana na utegemezi,” amesema Mhe. Munkunda.

Ameongeza kuwa, LATRA inafanya mabadiliko makubwa ya uendeshaji na udhibiti katika sekta ya usafiri ardhini kwa kushirikiana na wadau na kwa sasa inaonesha wazi kuwa sekta imeboreshwa na huduma zinatolewa kwa uwazi, uweledi na ufanisi huku wadau wakifurahia ushirikishwaji katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta yao.

Pia, amewapongeza viongozi wa KIBABOT SACCOS kwa kukubali na kufanyia kazi wazo la LATRA la kuanzisha ushirika ambao umekuwa wenye tija kwao kwa kuwawezesha kuinuana kijamii, kiuchumi na kuongeza fursa za uwekezaji kama ushirika pamoja na kupata fursa ya kukopeshana na kukopesheka kwa maendeleo ya wanachama na ushirika kwa jumla.

“Mmeniambia mnatanua wigo wa SACCOS yenu, natamani Wilaya ya Mwanga iwe ya kwanza kuwa na tawi la KIBABOT SACCOS, na maafisa wasafirishaji wa hapa wapo tayari kwa hilo nasi tunawaunga mkono,” amesisitiza Mhe. Munkunda.

>>>> *Inaendelea Uk. 20*

*<<<< Inatoka Uk. 19*

Mamlaka inafanya jitihada za kuwahimiza wamiliki na madereva wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda) na pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) kujiunga pamoja na kuanzisha vyama vya ushirika ili kuboresha hali zao za maisha kijamii na kiuchumi.



***Bi. Olipa Lwendo, Afisa Utawala LATRA akitoa elimu kwa madereva wa usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda) kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 18, 2025 viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.***




***CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA (wa nne kushoto) na DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA (wa nne kulia) wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mabalozi Waandishi wa Habari za LATRA kwenye semina ya kuwajengea uwezo wanahabari hao iliyofanyika ukumbi wa TARI Kibaha Pwani kuanzia Mei 6 hadi 7, 2025.***

# MHE. KHAMIS AKOSHWA NA BAJAJI ZINAZOTUMIA UMEME



***Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) akipatiwa elimu na Bw. Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA kuhusu pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) zinazotumia umeme zinavyotunza mazingira kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira iliyofanyika jijini Dodoma, viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete Juni 4, 2025.***

Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) amekoshwa na pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) kwa kuwa zinatumia nishati safi ya umeme na zinasaidia utunzaji wa mazingira.

Mhe. Khamis amesema hayo Juni 04, 2025 alipotembelea banda la LATRA na kupatiwa elimu ya jinsi pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) zinazotumia umeme zinavyotunza mazingira kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira iliyofanyika jijini Dodoma, viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete.

Vilevile Mhe. Khamis ametoa rai kwa wadau kununua pikipiki hizo kwa kuwa ni rahisi kutumia, ni rafiki kwa mazingira na zitasaidia kuinua vipato vyao kwa kuwa gharama za uendeshaji wake ni mdogo ukilinganisha na zile zilizozoeleka.

Akitoa elimu ya pikipiki hizo, Bw. Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA amesema kuwa, pikipiki hizo zinawekwa chaji kwa saa tatu na kwenda umbali wa kilomita 100 huku zikitumia umeme wa TZS. 3,000 tu. "Uwepo wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu zinazotumia umeme zinachagizwa na mapinduzi makubwa ya Teknolojia katika sekta ya usafiri nchini yanayoleta tija na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi na kuleta unafuu wa uendeshaji kwa wasafirishaji", amesema Bw. Silanda.

Naye Bi. Mercy Kitomari kutoka Kampuni ya TRI amesema kuwa, kampuni hiyo inazo pikipiki za magurumu mawili (bodaboda), magurudumu matatu (bajaji) na maguta yanayotumia umeme yataanza kupatikana nchini hivi karibuni.

LATRA inatekeleza kwa vitendo maono na maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye anasisitiza ushirikiano wa Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali ambapo katika maonesho ya Wiki ya Mazingira yaliyofanyika jijini Dodoma, Mamlaka kwa kushirikiana na Kampuni ya TRI inayomilikiwa na wazawa, wameonesha pikipiki za magurumu matatu zinazotumia umeme ambazo zinaongeza fursa kwa watoa huduma wa usafiri ardhini nchini.

# DCP KAHATANO: TUSHIRIKIANE KUTOKOMEZA RUSHWA



*Wadau wa usafirishaji wakiwa kwenye semina ya kukuza maadili na kupambana na rushwa iliyoandaliwa na Kamati ya Uadilifu ya LATRA kwa Taasisi zisizo za Kiserikali Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Mei 29, 2025.*

DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi wadau wa usafiri ardhini kushirikiana na LATRA katika jitihada za kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa ili kuwa na sekta ya usafiri ardhini yenye tija.

DCP Kahatano amebainisha hayo kwenye semina ya kukuza maadili na kupambana na rushwa iliyoandaliwa na Kamati ya Uadilifu ya LATRA kwa Taasisi zisizo za Kiserikali na kufanyika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Mei 29, 2025.

Katika semina hiyo, DCP Kahatano amesema kuwa, Mamlaka inakemea vikali vitendo vya rushwa na inatambua kuwa suala la kupambana na rushwa ni mtambuka hivyo ni muhimu kila mdau wa usafiri ardhini kutambua nafasi na wajibu wake kwa kukataa vitendo hivyo ambavyo vina athari kubwa katika utoaji wa huduma kwa watanzania.

"Tunatambua rushwa ni adui wa haki na ni matokeo ya ukiukwaji wa maadili, hivyo endapo kutakuwa na viashiria vyovyote vya vitendo vya rushwa LATRA, tunaomba muwasiliane nasi kwa kupiga simu bila malipo kwa namba 0800110019/20, kutumia mfumo wa emrejesho emrejesho.gov.go.tz/, baruapepe ya Mamlaka kwa anwani ya info@latra.go.tz au kuwasiliana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili hatua zichukuliwe kwa haraka.

Vilevile amesema, Serikali inatekeleza Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne wa mwaka 2023 – 2030 wenye lengo mahususi la kushirikisha sekta binafsi kwenye mapambano dhidi ya rushwa na kukuza uadilifu.

Mhandisi Eliud Kataraihya, Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) LATRA amesema Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anasisitiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA na kuhakikisha mifumo hiyo inabadilishana taarifa ambapo LATRA inatekeleza hilo kwa vitendo kwa kubuni na kutumia mifmo ya TEHAMA katika shughuli zake za kiudhibiti.

Ameongeza kuwa, Mamlaka inabuni na inatumia mifumo ya TEHAMA kutoa huduma kwa wadau wake ambapo kwa sasa wadau hao hawalazimiki kuonana na mtumishi wa Mamlaka pindi unapotaka kupata huduma, hali ambayo inasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti vitendo vya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji.

**>>>> *Inaendelea Uk. 23***

<<<< *Inatoka Uk. 22*

"Kwa upande wa madereva wa vyombo vinavyodhibitiwa na LATRA, kuna Mfumo wa Kutahini Madereva yaani DTS ambapo dereva anapofanya mtihani wa kuthibitishwa na Mamlaka, Mfumo ndio unachagua maswali, kusahihisha na kutoa alama.

Haya yote yanafanyika bila kuwa na mtu wa kati, kwa hiyo kwa mazingira haya, imesaidia kupambana na vitendo vya rushwa ambavyo vinadidimiza haki ya mdau", ameeleza Mha. Kataraihya.

Nae Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA amesema miongoni mwa jitihada zinazotekelezwa na LATRA za kupambana na rushwa ni kupitia utoaji wa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali ikiwemo redio, runinga, mitandao ya kijamii, kushiriki kwenye maonesho pamoja na mikutano mbalimbali ya wadau.

Kwa upande wake,Bi. Marcella Salu, Afisa Mchunguzi Mkuu kutoka TAKUKURU amesema rushwa ni adui wa haki na kila mmoja anawajibika kupambana na vitendo vya rushwa na kuvitolea taarifa kwa Mamlaka husika kwa kuwa vitendo hivyo vina madhara mengi ikiwemo kukwamisha utoaji wa haki, kuzorotesha mendeleo ya nchi, kutolewa kwa huduma duni au kukosekana kwa huduma, kudhoofisha nguvu kazi ya Taifa pamoja na kukosekana kwa amani na kuchochea chuki kwa wananchi.

Nao wadau waliohudhuria semina hiyo wameipongeza LATRA kwa kuwashirikisha katika masuala yanayohusu sekta ya usafiri ardhini na wameishukuru kwa kuwapatia elimu hiyo na wameahidi kuiwasilisha kwa wengine.

Semina hiyo imehudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TAMSTOA), Umoja wa wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA), Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Usafirishaji (TADWU), Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (CHAWAMATA), Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA) Pamoja na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC).



# LATRA YAANZA KUKAGUA UTEKELEZAJI WA SHERIA NA KANUNI ZA WAHUDUMU WA MABASI YA KIBIASHARA




***Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA akitoa taarifa kwa umma Jijini Dodoma Mei 17, 2025 kuhusu utekelezaji wa Sheria na Kanuni za udhibiti wa wahudumu kwa mabasi yote ya masafa marefu ambapo kuanzia Juni 2, 2025 adhabu zitaendelea kutolewa kwa wanaokiuka Sheria hizo.***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeanza kukagua utekelezaji wa Sheria na Kanuni za udhibiti wa wahudumu kwa mabasi yote ya masafa marefu na kuanzia tarehe 02 Juni, 2025 adhabu zitaendelea kutolewa kwa wanaokiuka Sheria hizo.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA kwenye taarifa iliyotolewa jijini Dodoma Mei 17, 2025. Katika taarifa hiyo Bw. Pazzy amesema Mamlaka inawakumbusha wamiliki wa vyombo hivyo kutekeleza matakwa ya kanuni ya 22(g) ya Kanuni za Magari ya Abiria za Utoaji wa Leseni za Usafirishaji Tangazo la Serikali Na. 76 la Mwaka 2020 inayomtaka mtoa huduma kuhakikisha mhudumu anaye mwajiri amesajiliwa na LATRA.

Ameongeza kuwa, kwa upande wa wahudumu nao wanatakiwa kutii kanuni ya 20(1)(d) ya Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili Wahudumu wa Magari ya Biashara za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tangazo la Serikali Na. 81 la Mwaka 2020 zinazomtaka mhudumu wa magari ya kibiashara kuwa na kadi ya usajili iliyotolewa na Mamlaka.

“Tunawakumbusha wahudumu wote kuwasilisha maombi ya kusajiliwa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) kwa anwani ya rrims.latra. go.tz au kufika ofisi za LATRA wakiwa na nakala ya Cheti cha Mafunzo na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) ili kusajiliwa na kupatiwa kadi ya usajili” amesisitiza Bw. Pazzy.

Vilevile ameeleza kuwa, katika kutekeleza takwa la Kisheria na Kanuni zake, mwezi Julai 2023, LATRA ilizindua mafunzo ya wahudumu wa mabasi na tarehe 14 Agosti, 2024 Mamlaka ilitangaza tarehe 31 Disemba, 2024 kuwa mwisho wa watoa huduma nchini kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na LATRA huku ikiendelea kutoa elimu na kuwezesha utekelezaji.

Mamlaka ilitangaza tarehe 31 Disemba, 2024 kuwa ni mwisho wa watoa huduma nchini kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na LATRA huku ikiendelea kutoa elimu na kuwezesha utekelezaji ambapo ilizindua mafunzo ya wahudumu wa mabasi Agosti 14, 2024 yanayotolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), na Chuo cha Ufundi Arusha kwa utaratibu wa kuwafikia wahitaji.

# MHE. KUNENGE AFUNGA RASMI SEMINA YA WANAHABARI MABALOZI WA LATRA



*Mhe. Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, akifunga rasmi semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), iliyoandaliwa na LATRA Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI - Kibaha Mkoa wa Pwani.*

Mhe. Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, amefunga rasmi semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA),huku akiwapongeza wanahabari hao kwa kuwa kinara kutenga muda wao kuhudhuria semina hiyo iliyoandaliwa na LATRA.

Pongezi hizo amezitoa Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI- Kibaha Mkoa wa Pwani ambapo Wanahabari Mabalozi 40 kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini walijengewa uwezo kuhusu uandishi wa habari za LATRA pamoja na kufahamu kazi na majukumu ya Mamlaka.

"Namshukuru CPA Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA kwa kunialika rasmi kufunga semina hii ambayo mmeiendesha hapa katika Mkoa wangu, jambo hili ni zuri naamini waandishi hawa wakitoka hapa watakuwa mahiri zaidi na watatumia kalamu zao vizuri katika kuelimisha jamii kuhusu masuala yanayohusu sekta ya usafiri ardhini nchini pamoja na jitihada za kuboresha sekta ya Usafiri Ardhini zinazotekelezwa na Serikali yetu ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan," amesema Mhe. Kunenge.

Mhe. Kunenge ameongeza kuwa, Mhe. Dkt. Raisi Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa ni kiongozi wa kuigwa kwa kuwa amekuwa kinara katika utendaji wa majukumu ya nchi ambapo amefanya jitihada kubwa kuboresha barabara mkoa wa Pwani zinazochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka kwa wananchi.

Vilevile, amempongeza CPA Suluo na Menejimenti yake kwa jitihada wanazozifanya katika udhibiti wa sekta ya usafiri ardhini nchini na pia kwa kuwa na uhusiano mzuri na wadau wakiwemo wanahabari ambao wamekuwa wakisaidia kufikisha taarifa za LATRA na Serikali kwa wananchi kwa wakati mwafaka.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA alimueleza Mhe. Kunenge kuwa, semina hiyo imeendeshwa kwa siku mbili yaani Mei 6 na 7, 2025 na Mamlaka itaendelea kufanya kazi kwa karibu na ushirikiano na wanahabari nchini kwa kuwa wanafanya kazi kubwa ya kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali yanayojenga Taifa na yanayoakisi maono na falsafa za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# CPA SULUO: MSIKUBALI KUSITISHA SAFARI MNAPOTUMIA HUDUMA ZA TAKSI MTANDAO



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akiwasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa LATRA Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI- Kibaha Mkoa wa Pwani.*

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi abiria wanaotumia huduma za taksi mtandao kutokubali kusitisha safari kabla ya kufika mwisho wa safari kwa kuwa ni hatari kiusalama.

CPA Suluo amesema hayo alipowasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa LATRA kuhusu uandishi wa habari za LATRA pamoja na kufahamu kazi na majukumu ya Mamlaka, Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI uliopo Kibaha Mkoa wa Pwani.

"Msikubali kusitisha safari pindi dereva wa taksi mtandao anakuomba kufanya hivyo kwa kuwa sio tu mnahatarisha usalama wenu, lakini pia mnapoteza mapato ya Serikali. Mnapokutana na changamoto hiyo, tupigieni simu bila malipo kwa namna 0800110019 au 0800110020 nasi tutashughulikia," amesema CPA Suluo.

Vilevile amesema, Mamlaka imetoa leseni za usafirishaji kwa kampuni 26 zenye Mifumo ya Taksi/ Pikipiki Mtandao ambapo hadi kufikia tarehe 07 Mei, 2025, kampuni zenye leseni ni 11 (42.3%), na ambao leseni zao zimeisha muda ni 15 (57.7%).

"Niwakumbushe wamiliki na watoa huduma za usafiri wa kukodi kuhakikisha kuwa wana leseni hai ya LATRA kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni kutoa huduma bila leseni ya mdhibiti na watakaokiuka Sheria hiyo watawajibishwa kwa kutozwa faini kama sehemu ya adhabu," amesema CPA Suluo.

Wakati huohuo CPA Suluo amesema, Mamlaka inawajibu wa kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma za usafiri na pia Mamlaka imetekeleza wajibu wa kupanga nauli za Teksi/Pikipiki Mtandao ili kulinda maslahi ya abiria, mwenye teksi/pikipiki pamoja na wenye mifumo ya teksi/pikipiki mtandao.

Kifungu cha 5(1)(g) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 kimeipa Mamlaka jukumu la kufuatilia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na salama na zenye viwango.

# LATRA YATOA LESENI 334,859 KWA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akielezea mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa leseni za usafirishaji za LATRA kwenye semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa LATRA Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI- Kibaha Mkoa wa Pwani.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa leseni 334,859 kwa vyombo vya moto kibiashara kuanzia mwaka 2021 hadi Machi 2025 kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Reli na Barabara (Railway and Road Information Management System - RRIMS) kwa anwani ya rrims.latra.go.tz amebainisha hayo CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA alipowasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye semina ya kuwajengea uwezo wanahabari Mabalozi wa LATRA kuhusu uandishi wa habari za LATRA pamoja na kufahamu kazi na majukumu ya Mamlaka, Mei 7, 2025 ukumbi wa TARI uliopo Kibaha Mkoa wa Pwani.

"Idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kwa vyombo vya usafiri wa abiria (passenger service vehicles), mizigo (goods carrying vehicles), na vyombo vya usafiri wa kukodi (private hire service vehicles) ziliongezeka kutoka **226,201** mwaka **2020/21** (Februari, 2021) hadi **334,859** mwaka **2024/25** (Machi, 2025), ikiwa ni ongezeko la leseni **108,658,** sawa na ongezeko la **asilimia 48,** Hili ni sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 12 kila mwaka katika kipindi cha miaka minne (4) inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan" amesema CPA Suluo.

Vilevile ameongeza kuwa Mfumo wa RRIMS unamuwezesha Msafirishaji kuchapa leseni yake popote alipo bila kufika ofisi za LATRA na unamwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 na hivyo kupunguza usumbufu na muda wa kupata huduma.

"RRIMS ni Mfumo mama wa Mamlaka ambao unasaidia katika utoaji wa leseni za magari ya abiria na mizigo, usajili wa madereva, malipo na taarifa za udhibiti na Mfumo huu umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA ili kurahisisha uhakiki wa leseni zinazotolewa na Mamlaka" amesema CPA Suluo.

Kifungu cha 5(1)(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 kimeipa Mamlaka jukumu la kutoa, kuhuisha, kusitisha na /au kufuta leseni za usafirishaji magari ya abiria na mizigo ambapo Mfumo wa RRIMS unafanikisha utekelezaji wa jukumu hilo.

# CPA SULUO AWASIHI WANAHABARI KUTUMIA VIZURI KALAMU ZAO



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akiwasihi Wanahabari Mabalozi wa LATRA kutumia vizuri kalamu zao katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu ili kulinda amani na utulivu wa nchi kwenye semina ya kuwajengea uwezo Wanahabari hao Mei 6, 2025 ukumbi wa TARI- Kibaha Mkoa wa Pwani.*

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi Wanahabari Mabalozi wa LATRA kutumia vizuri kalamu zao katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu ili kulinda amani na utulivu wa nchi.

CPA Suluo amesema hayo Mei 6, 2025 alipofungua rasmi semina kwa Wanahabari Mabalozi wa LATRA yenye lengo la kuwajengea uwezo wanahabari hao kuhusu uandishi wa habari za LATRA pamoja na kufahamu kazi na majukumu ya LATRA, iliyofanyika ukumbi wa TARI uliopo Kibaha Mkoa wa Pwani na kuhudhuriwa na wanahabari 40 kutoka vyombo mbalimbali vya habari pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya LATRA.

“Tunaelekea kwenye kipindi cha Uchaguzi Mkuu na jamii inategemea sana kupata taarifa kutoka kwenu. Nawaomba mtoe taarifa sahihi, zenye ukweli, zisizo na ubaguzi na bila upendeleo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani, umoja na mshikamano”, amesema CPA Suluo.

Ameongeza kuwa, LATRA inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wanahabari hao kwa Mamlaka katika kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Mamlaka na pia amesema ni matarajio ya Mamlaka kuwa uwepo wao utawezesha kujifunza na kuufikishia umma wa watanzania taarifa sahihi kuhusu juhudi kubwa za kuboresha sekta ya Usafiri Ardhini zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia LATRA,” amesema CPA Suluo.

“Natumia fursa hii kutoa Pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wenye mafanikio mengi makubwa katika Awamu hii ya Sita. Kwa uchache niseme uongozi wa Mhe. Dkt Samia umetujengea mazingira mazuri, bora na rafiki ya kusimamia sekta ya usafiri ardhini kwa weledi na ufanisi mkubwa tukizingatia sana ushirikishwaji wa wadau wetu wote muhimu” amesema CPA Suluo.

Kwa upande wake Bi. Ikunda Erick, mwandishi wa gazeti la *Habari Leo* ameishukuru LATRA kwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya LATRA na Wanahabari hao pamoja na kuwawezesha kushiriki katika semina ya kuwajengea uwezo na amewasihi wanahabari wenzake kuendelea

**>>>> *Inaendelea Uk. 29***

<<<< *Inatoka Uk. 28*

kutoa taarifa za kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hiyo ili wananchi wafahamu kwa kina kuhusu jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia LATRA.

Semina hiyo ya siku mbili inafanyika Mei 6 na 7, 2025 ambapo miongoni mwa mada zitakazowasilishwa ni Majukumu ya LATRA katika Udhibiti Usafiri wa Barabara, Nafasi ya TEHAMA katika Kuboresha Huduma za Usafiri Ardhini, Nafasi ya Wanahabari katika Kuboresha Huduma za Usafiri Ardhini, Mafanikio ya LATRA katika miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Udhibiti wa Usafiri wa Reli na Usafiri wa Waya pamoja na Nafasi ya Wanahabari katika Kutekeleza Sheria za LATRA.





***DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA akiongoza semina ya kukuza maadili na kupambana na rushwa kwa wadau wa usafiri kutoka taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali iliyofanyika ofisi za Dar es Salaam Mei 29, 2025.***

# LATRA YAFANYA KAGUZI 275 USAFIRI WA RELI



*Wataalamu kutoka LATRA wakikagua miundombinu ya reli pamoja na vitembea reli ikiwa ni pamoja na Treni ya Kisasa (SGR) baada ya kuwasili nchini na kabla ya kuanza kutoa huduma ili kujiridhisha usalama wake kisha kutoa ithibati.*

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema kuwa, kuanzia Februari, 2021 hadi Machi, 2025 Mamlaka imefanya jumla ya kaguzi 275 katika miundombinu ya reli, ishara na mawasiliano, vitembea reli (vichwa na mabehewa) na uendeshaji ambapo kati ya kaguzi hizo, 143 zilikuwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), na kaguzi 132 zilikuwa kwa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

CPA Suluo, amesema hayo alipoelezea mafanikio ya LATRA ndani ya miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Chuo cha Taifa cha Utalii, Dar es Salaam.

Amebainisha kuwa, wataalamu kutoka LATRA wamefanya kaguzi mbalimbali za miundombinu ya Reli pamoja na vitembea reli ikiwa ni pamoja na Treni ya Kisasa (SGR) baada ya kuwasili nchini na kabla ya kuanza kutoa huduma ili kudhirisha usalama wake kisha kutoa ithibati.

Kwa upande wa uanzishwaji wa huduma za Treni za SGR, CPA Suluo amesema katika maandalizi ya kuanza kwa huduma za usafiri wa abiria kwa treni za SGR, Mamlaka ilikuwa na jukumu la kuthibitisha ubora wa vitembeareli kabla ya kuanza kutoa huduma.

“Tuliungana na timu ya wataalamu wa TRC na Wizara ya Uchukuzi kwenda Nje ya Nchi kukagua na kuthibitisha ambapo jumla ya vichwa vya treni 17, Mabehewa ya abiria 56, treni za seti za umeme (EMU) 10 na Mabehewa ya mizigo 264 yamekaguliwa kipindi cha uundwaji katika nchi za Korea, China, Malaysia na Ujerumani. Pia Mamlaka imefanya kaguzi za majaribio kwa mabehewa na vichwa hivyo baada ya kuwasili nchini kabla ya kuanza kutumika kutoa huduma,” amefafanua CPA Suluo.

Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya usafiri ardhini nchini ikiwemo usafiri wa reli ambapo tumeshuhudia uanzishwaji na uendeshwaji wa treni za kisasa (SGR) uliozinduliwa rasmi jijini Dodoma Agosti 1, 2024 na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Usafiri huu umechochea ongezeko la uchumi wa wananchi na Serikali kwa jumla na umekuwa ni usafiri salama na unaoaminika uliochagizwa na kaguzi zinazofanywa na LATRA kwa uweledi na ufanisi hivyo kuongeza tija ya huduma za usafiri huu nchini.

# CPA SULUO: HATUPANGI NAULI ZA DARAJA LA KIFAHARI




***CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akiwasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye Mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.***

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema kuwa, LATRA haipangi nauli za daraja la kifahari (VIP/VVIP/Royal Class) za mabasi ya masafa marefu na treni za kisasa (SGR) bali inapanga nauli za daraja la kawaida zinazozingatia hali za watanzania ili waweze kumudu gharama za usafiri nchini.

CPA Suluo amebainisha hayo alipowasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye Mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.

"Jukumu la LATRA ni kuhakikisha watanzania wanazipata hizi huduma na wanazifikia kwa kuzingatia zaidi wale wenye pato la chini na la kati, Mamlaka imeruhusu wasafirishaji kujipangia nauli za daraja la biashara (Business Class) na madaraja mengine ya juu (Royal Class) kwa kuwa eneo hili ni kwa abiria wenye uwezo kifedha na wanaoweza kufikia huduma hii ili kuruhusu ushindani kwa wasafirishaji," amesema CPA Suluo.

CPA Suluo ameongeza kuwa, LATRA imetekeleza jukumu la kisheria kwa kupanga nauli za daraja la uchumi (Economy Class) wakati wa uanzishwaji wa huduma za treni ya kisasa (SGR), jukumu hili limetekelezwa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA.

"Ni jukumu letu kupanga nauli za usafiri huu na kwa daraja la kawaida na tumewazingatia Wananchi wa kawaida kwani watazimudu nauli hizi ambapo kwa treni itakayokuwa inasimama kila kituo ni shilingi 13,000 kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro na shilingi 31,000 kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo watoto chini ya miaka minne hawatalipia gharama hizo na watoto wenye umri wa miaka minne hadi 12 watalipia nusu gharama ya nauli hizo na nauli hizi zipo katika tovuti yetu www.latra.go.tz" ameeleza CPA Suluo.

Katika Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, LATRA inaendelea kushirikiana na wadau wengine wa usafiri ili kuhakikisha huduma bora na salama kwa wananchi wote na Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuboresha sekta ya usafiri kwa kuunganisha mikoa mbalimbali nchini.

# LATRA YASOGEZA HUDUMA ZA USAFIRI KARIBU NA WANANCHI




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA akizungumza na wanahabari na wahariri wa vyombo vya habari kwenye Mkutano ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kusogeza huduma za usafiri ardhini karibu na wananchi kwa lengo la kuboresha sekta ya usafiri nchini.

Amebainisha hayo CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, alipowasilisha mafanikio ya LATRA katika Miaka Minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye Mkutano na Wahariri na Waandishi wa Habari ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Aprili 14, 2025, Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam.

"Tumefungua ofisi kumi (10) maeneo ya kimkakati kwenye baadhi ya Halmashari za Miji na Wilaya nchini. Maeneo hayo ni Kituo cha Mabasi Magufuli - Mbezi, Tegeta, na Mbagala (Dar es Salaam), Makambako (Njombe), Kahama (Shinyanga), Masasi (Mtwara), Ifakara (Morogoro), Korogwe (Tanga), Same (Kilimanjaro), na Nzega (Tabora)," amesema CPA Suluo.

CPA Suluo ameongeza kuwa, Mamlaka inaendelea na juhudi za kusogeza huduma za LATRA karibu na wananchi na taratibu za kuanzisha Ofisi nyingine tano (5) zinaendelea katika maeneo ya Gongo la Mboto Mkuranga (Pwani), Chunya (Mbeya), Mufindi (Iringa), na Nyakanazi (Kagera).

Vilevile CPA Suluo ameeleza jinsi ofisi ndogo za Mamlaka zilizvyowafikia wananchi na wadau, "kufikia mwezi Machi 2025, ofisi hizi ndogo zimeonesha mafanikio katika kufikia wananchi walio mbali na miji mikuu ya mikoa, kuboresha udhibiti wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda), kutatua migogoro ya wadau katika maeneo hayo, kufikisha elimu kwa wadau na kusogeza ushirikiano na mamlaka mbalimbali kwenye maeneo hayo, ikiwemo Serikali za Mitaa (LGAs), Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na mamlaka zingine zilizopo kwenye maeneo hayo.

Wakati huohuo, CPA Suluo ameeleza kuwa Mamlaka imeendelea kusogeza huduma za usafiri wa miji na majiji karibu na wananchi katika maeneo yenye changamoto za usafiri kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa.

"LATRA imeendelea kuboresha usafiri wa umma katika miji na majiji makubwa hapa nchini, na imeanzisha njia mpya 1,007 za daladala Mkoani Dar es Salaam ili kufika maeneo yasiyofikika na kurefusha baadhi ya njia kwa lengo la kumpunguzia gharama mwananchi vilevile katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Arusha imefanya mabadiliko ya njia za daladala kwa kuzifanya baadhi ya njia kuwa za mzunguko kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma kwenye baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa na huduma," ameeleza CPA Suluo.




KW

# MAAFISA USAFIRISHAJI WILAYANI KASULU WAASWA KUZINGATIA SHERIA



*Wadau wa usafirishaji wakiwa kwenye semina ya yakuwajengea uelewa kuhusu vyama vya ushirika iliyofanyika Juni 21, 2025, ukumbi wa Shule ya Sekondari Bogwe, Wilayani Kasulu, Kigoma.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewasihi maafisa wasafirishaji Wilayani Kasulu, Mkoa wa Kigoma kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za usalama barabarani pamoja na Miongozo ya usafirishaji nchini.

Hayo yameelezwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, aliyemuwakilisha CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA kwenye Semina kwa Maafisa Wasafirishaji iliyolenga kuwapatia elimu ya vyama vya ushirika iliyofanyika Juni 21, 2025, ukumbi wa Shule ya Sekondari Bogwe, Wilayani Kasulu, Kigoma.

“Kazi yenu ya usafirishaji ni kama kazi nyingine, mnapaswa kujali uhai wenu na wa watu wengine kwa kufuata Sheria zilizopo. Pia, mnapaswa kuwa na leseni za usafirishaji ili mtekeleze kazi zenu kwa uhuru, kujiamini na hatimaye kujipatia kipato kitakachoendesha maisha yenu,” amesema Bw. Pazzy.

Ameongeza kuwa, suala la usalama wao kama wasafirishaji pamoja na abiria wanao wasafirisha ni muhimu, hivyo wanapaswa kuhakikisha wanakuwa na kofia ngumu wanapakia abiria mmoja kwenye pikipiki, kuvaa mavazi na viatu vinanayokidhi usalama wao wakiwa kwenye kazi zao za usafirishaji.

Naye Bw. Addo Msigala, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Kigoma amewaeleza maafisa wasafirishaji hao kuwa, Wilaya ya Kasulu ina pikipiki zaidi ya 3,000 lakini waliokata leseni LATRA ni 302 jambo ambalo linaonesha hali ya ukataji wa leseni Wilayani hapo kuwa mdogo na hivyo amewaasa kubadilika na kukata leseni hizo kupitia ofisi ya Posta ambao ni Mawakala wa ukataji leseni za LATRA Wilayani hapo.

Akitoa elimu ya usalama barabarani SP Damas Patrick, Mkuu wa Usalama Barabarani Wilayani Kasulu amewasihi maafisa wasafirishaji hao kutopandisha mtoto chini ya miaka 9 kwenye pikipiki bila kuwa na mtu mzima kwa kuwa ni kosa kisheria na inahatarisha usalama wa mtoto.

Vilevile SP Patrick amewakumbusha maafisa wasafirishaji hao kuzingatia mwendokasi uliowekwa wa kuendesha pikipiki kwa mwendo usiozidi kilometa 50 kwa saa, kuzingatia alama na ishara za barabarani, chombo kuwa na matairi bora, pikipiki kuwa na vioo vya kutazama nyuma (side mirrors) pamoja na kuacha kutumia simu wakiwa kwenye shughuli zao za usafirishaji.

Semina hiyo imeratibiwa na Mhe. Joyce Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini na kuhudhuriwa na maafisa wasafirishaji waliopatiwa elimu ya usalama barabarani, ukataji wa leseni za LATRA, Hali ya huduma za usafirishaji Wilayani Kasulu, Elimu ya vyama vya ushirika, faida zake, taratibu za kujiunga na vyama vya ushirika.

# TANZANIA KUNUFAIKA NA FURSA ZA USAFIRISHAJI SADC



*Mhe. Prof Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi (wa tatu kushoto) kwenye picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wakati aliposhiriki Mkutano wa Nne wa Usafirishaji na Lojististiki kwa nchi zinazopitisha Shehena Zambia katika Ukanda wa SADC (Land-Linked Zambia 4th Conference). Uliofanyika Lusaka, Zambia kwa siku mbili kuanzia tarehe 10 hadi 11 Aprili, 2025.*

Mhe. Prof Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, ameshiriki katika Mkutano wa Nne wa Usafirishaji na Lojististiki kwa nchi zinazopitisha Shehena Zambia katika Ukanda wa SADC (Land-Linked Zambia 4th Conference). Mkutano huo umefanyika Lusaka, Zambia kwa siku mbili kuanzia tarehe 10 hadi 11 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia alikuwa Mgeni Rasmi na Mkutano umehudhuriwa na Mawaziri kutoka nchi za SADC, wawekezaji, wafadhili, wasafirishaji na wadau mbalimbali wa usafirishaji na lojistiki.

Akifungua Mkutano huo, Mhe. Hichilema alisisitiza Umoja, ushirikiano wa kiuchumia, shughuli za kibiashara na uwekezaji katika Nchi za SADC bila kujali mipaka ya kijiografia.

Lengo la mkutano huo ni kuwakutanisha wadau mbalimbali wa usafirishaji na lojistiki katika nchi za SADC hususan shoroba mbalimbali ambazo zinatumiwa na nchi ya Zambia kupitisha shehena ya mizigo. Wadau hawa wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu na fursa zilizopo katika Nchi zao.

Katika Mkutano huo Mhe. Waziri Mbarawa alipata fursa ya kutoa maelezo na kuitangaza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu fursa mbalimbali za Uwekezaji katika sekta ya Usafiri na Usafirishaji kupitia shoroba zinazoiunganisha Tanzania na nchi za SADC.

Uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali hususan katika Bandari, Reli ya SGR, TAZARA, Ujenzi wa Meli katika Maziwa Makuu na Uwepo wa Ndege ya Mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 54 ni maeneo muhimu Mheshimiwa Waziri atakayotolea taarifa katika mkutano huo. Katika ziara hiyo, Mhe. Mbarawa ameambatana na viongozi mbalimbali akiwemo CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA.

# MADEREVA ARUSHA WAHIMIZWA KUSAJILIWA NA KUTHIBITISHWA NA LATRA



*Bw. Omary Saleh, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Arusha akitoa elimu ya usajili na uthibitishaji wa madereva wa vyombo vya moto kibiashara kwa maafisa usafirishaji jijini Arusha.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewahimiza madereva wa vyombo vya moto kibiashara kujisajili na kuthibitishwa na LATRA kama illivyoainishwa kwenye Kanuni ya (4)(1) ya Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu ya mwaka 2020.

Bw. Omary Saleh, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Arusha amesema hayo hivi karibuni alipotoa elimu ya usajili na uthibitishaji wa madereva wa vyombo vya moto kibiashara jijini Arusha.

“Taratibu za kusajiliwa ni rahisi sana kama unasimu janja unaweza kuingia katika Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) na utaingiza taarifa zako za NIDA kisha utaambatisha cheti cha udereva na leseni ya udereva. Lengo ni kupata taarifa za kumbukumbu za madereva waliosajiliwa na kuthibitishwa na LATRA na Mamlaka itaweza kutambua makosa ya dereva husika anayeendesha chombo kwa wakati huo,” ameeleza Bw. Saleh.

Vilevile Bw. Saleh ameeleza kuwa Mamlaka imeweka mazingira rafiki yanayo muwezesha dereva kufanya mtihani wa uthibitishaji.

“Utaratibu uliowekwa kulingana na mazingira Serikali imezingatia ambapo mtihani huo hufanywa kwa lugha mama ya kiswahili ili madereva wapate kuelewa na maswali yanayo ulizwa ni ya kupima uelewa wa dereva na mfumo ni rahisi unaomuwezesha dereva kujibu maswali bila kupata changamoto yoyote.”

Pia, Bw. Saleh alitoa elimu ya matumizi sahihi ya Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i- Button) kwa madereva wa magari maalum ya kukodi (Special Hire) wanachopatiwa baada ya kuthibitishwa na Mamlaka ambapo amewaeleza madereva hao kuwa i-Button ni mali ya dereva na sio mmiliki na wanapaswa kukitumia wakati wote wa safari ili kupata taarifa za dereva husika pamoja na kutambua mwenendo wake akiwa safarini.

Naye Bw. Ernest Mmasi, dereva wa mabasi ya mjini (daladala) kituo cha daladala Kilombero Jijini Arusha ameishukuru Mamlaka kwa jitihada za kuwapatia elimu ya usajili na uthibitishaji na wameona ni jambo lenye tija na litawaongezea heshima na kutanua wigo wa ajira ya fani hiyo.

“Jambo hili lilikuwa linanitatiza kwa kuwa hatukuwa na uelewa wa kwanini tunalazimika kufanya mtihani wa LATRA hali ya kuwa madereva wameshafanya mtihani wa VETA na kupatiwa leseni halali, baada ya kupata elimu hii kwa sasa nimeelewa na nitakuwa balozi mzuri kwa wenzangu kwa kuwa

**>>>> Inaendelea Uk. 37**

<<<< *Inatoka Uk. 36*

hamasisha kwenda ofisi za LATRA na kufanya mtihani wa uelewa na hatimaye na sisi tuthibitishwe na kutambulika na Serikali," amesema Bw. Mmasi.

Bw. Salum Kondo, dereva wa lori Jijini Arusha amewaasa madereva wenzake kwenda kusoma elimu ya udereva kwenye vyuo vinavyotambulika na Serikali ili wapate vyeti vya taaluma hiyo na hatimaye waende LATRA kwa ajili ya kuthibitishwa.

Kwa upande wake, Bw. Humphrey Pallanjo, dereva wa magari maalum ya kukodi jijini Arusha ambaye amesajiliwa na kuthibitishwa na LATRA amesema mtihani wa LATRA sio mgumu jambo la muhimu ni kufanya maandalizi ya kutosha kwa kujisomea na kujikumbusha yale uliyoyasoma chuoni.

Naye Bw. Salum Kivuyo dereva wa magari maalum ya kukodi Arusha amewasihi madereva wa magari maalumu ya kukodi kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Usafiri Ardhini ikiwemo kutumia kwa usahihi kitufe cha utambuzi wa dereva (i-Button) kwa kuwa manufaa yake ni makubwa hasa kwa upande wa usalama wa safari.

Mamlaka inaendelea kuwahimiza madereva wa vyombo vya moto kibiashara kusajiliwa ili kuthibitishwa kwa kuwa jambo hilo ni la kisheria lakini pia linaongeza thamani ya fani yao ya udereva. Baada ya kuthibitishwa, dereva atapatiwa cheti kinachotambulika kitaifa na kimataifa hasa kwa nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), hivyo ni manufaa makubwa kwa kuwa wanaenda kutanua wigo wa ajira ndani na nje ya nchi hatimaye watajiinua kiuchumi na kijamii.



# MADEREVA NA WAMILIKI WAHAMASISHWA KUJIUNGA NA VYAMA VYA USHIRIKA



*Bw. Omary Saleh, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Arusha akitoa elimu kwa wadau kuhusu taratibu na umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewahamasisha wamiliki na madereva wa pikipiki za Magurumu mawili (Bodadoda), pikipiki za Magurudumu matatu (Bajaji) pamoja na magari ya mijini (Daladala) kuanzisha vyama vya ushirika kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Bw. Omary Saleh, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Arusha alipo watembelea wadau hao na kuwapatia elimu ya taratibu na umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika.

Bw. Saleh amewaeleza wadau hao kwamba, kwenye huduma ya usafirishaji Serikali imewaletea ushirikishaji wa pamoja ambao utawasaidia kufanya mambo makubwa kwa pamoja ikiwemo kuboresha sekta ya usafirishaji na kukuza uchumi wa mmoja mmoja.

“Niwasihi tuungane na tushirikiane kufanikisha jambo hili lenye manufaa makubwa kwa kila mmoja wetu ukizingatia kuwa suala hili la ushirika limeletwa na viongozi wetu na kuwafikia ninyi kwa kuwashirikisha ili mkiona linafaa lifanyiwe kazi kwa kuweka utaratibu mzuri kwa Mamlaka na kwenu wadau kwa kufuata vigezo kama vile kuzingatia huduma inayotolewa kwa pamoja,” amesema Bw. Saleh.

Naye Bw. Pascal John, Afisa Usajili wa ushirika kutoka jiji la Arusha amebainisha taratibu za kufuata kujisajili kwenye umoja wa vyama vya ushirika, “Jambo la ushirika linataratibu zake na sisi tumekamilisha taratibu hizi ikiwemo kuwa na wazo la ushirika na kuwapatia elimu ya ushirika vilevile kuna vigezo vya kuzingatia ili kujiunga kwenye ushirika ikiwemo chama kuwa na washirika wasiopungua idadi ya watu 20 na wawe katika eneo husika kwa pamoja”.

Kwa upande wake Bw. Okelo Constantine, Mwenyekiti Umoja wa Bodaboda Mkoa wa Arusha (UBOMA) amesema kuwa, suala la ushirika kwa Mkoa wa Arusha wamelipokea vizuri na wanaamini utasaidia kufanikisha malengo waliyojiwekea ndani ya umoja wao.

“Tupo kwenye hatua za awali za kuandikisha ushirika na baada ya hapo tunapeleka mambo yetu kwa pamoja LATRA na baadae tutakabidhiwa hati na kuingia nao mkataba kama vile ukataji wa leseni za LATRA na tutapata gawiwo litakalotuwezesha kutekeleza mipango na maono ya ushirika wetu” ameeleza Bw. Constantine.

**>>>> *Inaendelea Uk. 39***

**<<<< Inatoka Uk. 38**

Aidha, Bw. Constantine amewaasa wamiliki wenzake kujitokeza kwa wingi kujiunga kwenye ushirika ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Ushirika huu ni fursa na tunaendelea kuwa hamasisha wanachama na bodaboda wote ndani ya Mkoa wa Arusha wajitokeze kwa wingi kujiunga na huu ushirika kwa sababu tutanufaika na kuboresha hali zetu za maisha kwa kufungua miradi mbalimbali tutakayoiendesha wenyewe kwa ushirika wetu" amesema Bw. Constantine.

Bw. Bill Albano, Mwenyekiti Umoja wa Daladala Jiji la Arusha (UWADAJA) amewaasa madereva na wamiliki wa daladala kujiunga kwenye ushirika kwakuwa unamanufaa makubwa kwao na wao kama wamiliki wapo tayari kufanya nao kazi kwa pamoja ili waweze kuinuana kiuchumi na kijamii.

Mamlaka inaendelea kuwapatia elimu ya uanzishwaji wa vyama vya ushirika kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kibiashara kwa kuwa itawasaidia katika kutekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi, itakuwa rahisi kwa Mamlaka kuwaratibu wakiwa katika majukumu yao, itawasaidia kukua kiuchumi na kuweza kusaidiana wao wenyewe na kikubwa zaidi itaongeza heshima ya kazi wanayoifanya.

Vilevile vyama vya ushirika vitawawezesha kupata fursa ya kujiwekea taratibu za utoaji huduma za usafirishaji, kupata mitaji kwa ajili ya kuboresha au kuongeza huduma pamoja na kupata elimu ya mara kwa mara ya biashara, usalama barabarani na masuala mengine na kukopeshana vitendea kazi.



# MAAFISA USAFIRISHAJI KASULU WAPOKEA FURSA YA VYAMA VYA USHIRIKA



*Mhe. Prof. Joyce Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini akiongoza semina iliyoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Juni 21, 2025 ukumbi wa Shule ya Sekondari Bogwe, Kasulu Mkoani Kigoma kuhusu umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika na faida zake.*

Maafisa usafirishaji Wilayani Kasulu Mkoa wa Kigoma wamesema wapo tayari kujiunga na kuanzisha chama cha ushirika kitakacho wawezesha kujiinua kiuchumi na kijamii kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Maafisa wasafirishaji wamebainisha hayo kwa nyakati tofauti baada ya kupatiwa semina ya umuhimu wa vyama vya ushirika na faida zake iliyoratibiwa na Mhe. Prof. Joyce Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini na kutolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Juni 21, 2025 ukumbi wa Shule ya Sekondari Bogwe, Kasulu Mkoani Kigoma.

"Elimu hii imetufumbua fikra kwamba kumbe tunaweza kujiunga, kuchagua viongozi na kuanzisha umoja wetu kupitia chama cha ushirika ambacho tunaweza kufika mbali kimaendeleo na kuepukana na hali ya umasikini," amesema Bw. Ally Shabari.

"Tunawashukuru LATRA kwa kutupatia elimu hii na tunaahidi kuendelea kupeana elimu kwa wenzetu ambao hawakufanikiwa kufika ili kwa pamoja tuunde ushirika wetu ambao kwa mujibu wa haya tuliyoelezwa na kuyaona kwa wenzetu wa KIBABOT kule Kilimanjaro na UWAMWA Mwanza, nasi imetupa mori na morali ya kuanzisha ushirika wetu ili nasi tuweze unufaika na faida mbalimbali zitakazotuwezesha kufika mbali kimaendeleo," amesema John Mselem.

Akizungumza katika semina hiyo, Mhe. Joyce Ndalichako Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini amesema kuwa, ameona ni wakati sahihi wa kutumia fursa hiyo inatolewa na Serikali kupitia LATRA na lengo lake ni kuhakikisha maafisa wasafirishaji hao wananufaika na fursa hiyo ya uchumi itakayowawezesha kubadili mustakabali wa maisha yao na familia zao.

"Wataalam wa LATRA wamewapatia elimu hii ya ushirika, Afisa Ushirika nae amewapa taratibu za kuanzisha ushirika, mimi nipo pamoja na nyie kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Lakini pia Jeshi la Polisi limetukumbusha kuhusu kutekeleza majukumu yenu kwa kufuata taratibu za usalama barabarani, wakati tunaendelea na mchakato wa kuanzisha ushirika basi mfuate Sheria zilizopo," ameeleza Mhe. Ndalichako.

Naye Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, aliyemuwakilisha CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA kwenye Semina

**>>>> *Inaendelea Uk. 41***

<<<< Inatoka Uk. 40

hiyo amesema kuwa, kazi ya kuendesha bodaboda ni kama kazi nyingine, hivyo amewakumbusha maafisa wasafirishaji hao kuheshimu, kuonesha weledi wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao na kutoa huduma bora huku wakizingatia usalama wao na abiria wanaowasafirisha.

Akizungumzia faida za vyama vya ushirika kwa maafisa usafirishaji hao, Bw. Pazzy amesema kuwa Mamlaka itawarejeshea kamisheni ya asilimia 20 ya pesa zitakazo patikana baada ya kukata leseni za LATRA kwa kuwa wata kuwa ni mawakala wa Mamlaka  na watakuwa na nguvu ya kusimamiana wenyewe katika majukumu yao.

Naye SP Patrick Damas amewakumbusha maafisa wasafirishaji hao kuzingatia mwendokasi uliowekwa wa kuendesha pikipiki kwa mwendo usiozidi kilometa 50 kwa saa, kuzingatia alama na ishara za barabarani, chombo kuwa na matairibora, pikipiki kuwa na vioo vya kutazama nyuma (side mirrors) pamoja na kuacha kutumia simu wakiwa kwenye shughuli zao za usafirishaji.

Kanuni za LATRA za Usafiri wa Magari ya Kukodi, 2020 ilifanyiwa marekebisho Machi, 2023 na kuruhusu LATRA kukasimu madaraka ya kutoa leseni kwa Wakala aliyethibitishwa ambao ni Vyama Ushirika, Taasisi za Umma (LGA), Kampuni na Watu Binafsi.



*Mhe. Joyce Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini akiongoza semina ya Maafisa wasafirishaji kuhusu elimu ya umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika iliyofanyika Juni 21, 2025 ukumbi wa Shule ya Sekondari Bogwe, Wilayani Kasulu, Kigoma.*

## MAFANIKIO YA LATRA KATIKA MIAKA MINNE (4) YA AWAMU YA SITA

Sekta ya usafirishaji inamchango mkubwa kwa ukuaji wa uchumi. Ili kuchochea zaidi maendeleo haya, mwaka 2019, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Lengo kuu lilikuwa ni kudhibiti huduma za usafiri ardhini kupitia barabara, reli, na usafiri wa waya.

Tangu kuanzishwa kwake, LATRA imeleta mabadiliko makubwa na kutatua changamoto zilizokuwepo awali, ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za usafiri wa umma.

Mafanikio ya LATRA yamewezeshwa na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Uchukuzi.

Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na ubunifu katika udhibiti wa usafiri, hali inayoongeza uwekezaji na kuwezesha mitaji kuwa endelevu. Wizara ya Uchukuzi chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akisaidiwa na Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi na Bw. Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi wamefanya jitihada za makusudi kuhakikisha Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa kusimamia vizuri sekta ya usafirishaji nchini na wadau kupata huduma bora, na katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 ambapo LATRA ilianzishwa hadi sasa, Mamlaka imepata mafanikio makubwa kupitia utekelezaji wa majukumu yake yakila siku.





# HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

## Safari za mabasi kwa saa 24

Serikali kupitia LATRA imeanzisha tena huduma za mabasi kwa saa 24 kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2024 baada ya kuzingatia maoni ya wadau na hali ya usalama barabarani. Hatua hii imeimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja, wasafirishaji, na Serikali kwa jumla kwa kuwa huduma hizo zimerahisisha ratiba za abiria kijamii na kibiashara.

Tangu kuanza kwa huduma za usafiri wa 24/7, LATRA imeendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani katika uratibu wa huduma za usafiri wa mabasi kwa kuimarisha usimamizi wa masharti ya leseni ikiwemo ukaguzi wa mabasi, utambuzi wa madereva kwa i-buttons na kongeza matumizi ya VTS. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2025, mabasi 2,323 yalikuwa yamepatiwa ratiba za kutoa huduma za usafiri usiku na mchana (24/7).

Aidha, tathmini ya LATRA ya mwaka mmoja wa utekelezaji wa ruhusa hii ya safari za usiku na mchana (24/7) umeonesha Wananchi wengi wamefurahishwa na kuridhishwa na maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kuondoa zuio la mabasi kusafiri usiku. Aidha, kuna mwitikio mkubwa wa Wananchi kutumia usafiri wa usiku kuliko mchana, na msongamano wa abiria kwenye Stendi umepungua sana, na 'mchezo' wa mabasi kukimbizana umepungua sana na unaelekea kwisha kabisa. Vilevile, tathmini ya LATRA inaonesha kuwa safari hizi za 24/7 zimepunguza gharama za njiani kwa abiria na kuboresha matumizi ya muda wao kwenye shughuli za kiuchumi, kijamii na kujiongezea vipato.

## Utoaji wa Leseni kwa Vyombo vya Moto kibiashara

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)( b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, LATRA ina wajibu wa kutoa, kuhuisha, kusitisha na/au kufuta leseni za usafirishaji, katika kufanikisha hili idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa ziliongezeka kutoka **226,201** mwaka **2020/21** (Februari, 2021) hadi **334,859** mwaka **2024/25** (Machi, 2025), ikiwa ni ongezeko la leseni **108,658,** sawa na ongezeko la **asilimia 48.**

Hili ni sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 12 kila mwaka katika kipindi cha miaka minne (4) inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

## Uthibitishaji wa Madereva na usajili wa Wahudumu

LATRA ina jukumu la kusajii wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya usafirishaji vinavyodhibitiwa. Lengo ni kuwa na madereva na wahudumu wenye weledi ili kufanikisha usalama wa huduma za usafiri wa umma na mizigo.

## Uthibitishaji wa Madereva

Mamlaka imeendelea kusajili na kuthibitisha madereva na kuwapatia Kitufe cha Utambuzi (i- Button) ili kufuatilia mienendo yao wawapo safarini kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS). Jumla ya madereva 8,172 wamesajiliwa na kupatiwa i- Button na madreva 9,191 waliofanya mtihani wa kuthibitishwa kati yao madereva 4,563 walifaulu mtihani huo na kupatiwa vyeti vya ufaulu.





## Usajili wa Wahudumu

Mamlaka ilizindua rasmi mtaala wa kufundishia wahudumu wa mabasi tarehe 1 Julai, 2023 kwa kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Chuo cha Ufundi Arusha ambapo hadi mwezi Mei, 2025, jumla ya wahudumu 1,940 wamepatiwa mafunzo na katiyao wahudumu 1,009 wamesajiliwa.

## Utengenezaji wa Kanuni mpya na ushirikishwaji wa Wadau

LATRA pia imefanikiwa kutengeneza na kutangaza kanuni mpya za usafiri ardhini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Ushirikishwaji wa sekta binafsi umekuwa muhimu katika masuala yanayowahusu wadau yana shughulikiwa kwa pamoja. Miongoni mwa fursa zilizowezeshwa na kanuni mpya za mwaka 2023 na 2024 ni pamoja na kuruhusu mawakala wa kutoa leseni za LATRA na kujipatia kipato kwa kurejeshewa 20% ya mapato yatokanayo na leseni husika na kuweka utaratibu wa kutoa onyo kabla ya adhabu kwa baadhi ya makosa katika huduma za usafiri.

Hadi sasa fursa hizo zimeanza kuwanufaisha wadau ambapo Chama cha Akiba na Mikopo cha KIBABOT Mkoani Kilimanjaro kinaendelea na utoaji wa leseni za LATRA kwa wanachama wake tangu mwanzoni mwa mwaka 2024 baada ya kupewa cheti cha ridhaa ya kutoa leseni za usafiri wa pikipiki, usafiri wa taksi na magari maalum ya kukodishwa.

## KUONGEZEKA KWA MAPATO

Mapato ya Mamlaka yameendelea kuongezeka ambapo kati ya mwaka wa fedha 2021/22 na 2023/24, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kwa asilimia 24.6, huku sehemu ya mapato hayo ikichangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, LATRA imekuwa ikipata hati safi kila mwaka kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), ikionesha uwajibikaji wa hali ya juu.



# KUKUZA MATUMIZI YA TEHAMA KWENYE UTOAJI WA HUDUMA

Serikali imeendelea kuiwezesha Mamlaka kubuni na kutengeneza Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imekuwa ikitumika katika shughuli mbalimbali za kiudhibiti. LATRA imeonesha mafanikio makubwa katika kudhibiti na kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini Tanzania, huku ikichangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mafanikio haya ni matokeo ya uwajibikaji wa hali ya juu na ushirikiano wa karibu kati ya Mamlaka, Serikali, na wadau wa sekta ya usafirishaji.

## Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS)

LATRA inazingatia ubunifu na haswa matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa kazi. Katika kipindi hiki, LATRA imejenga mfumo wa TEHAMA unaojulikana kama Railway and Road Information Management System (RRIMS) ambao ni mfumo mkuu wa utoaji leseni, usajili madereva, malipo na taarifa za udhibiti. Mfumo wa RRIMS umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA ili kurahisisha uhakiki. Kadhalika, Mfumo huu unamwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 bila uhitaji wa kufika ofisi za LATRA, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa usumbufu na muda wa kupata huduma.

## Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) – Safari Tiketi

LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya SerikaliMtandao (eGA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) pamoja na wadau wengine tumeunda mfumo jumuishi uliounganishwa na mifumo mingine ya utoaji tiketi ukiwemo wa TRC na mifumo ya tiketi za mabasi ili

kurahisisha ukataji tiketi na kutunza taarifa za abiria.

Katika kutekeleza Mfumo huu (CeTS) ambao unaweka Stendi za Mabasi na Treni Kiganjani, LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na Watoa Huduma wa Tiketi za Kielektroniki (e-Ticketing Vendors), imekamilisha kuunganisha Mifumo ya e-Ticketing ya TRC (MGR,SGR), pia imeunganisha mifumo ya e-Ticketing Vendors 13, na wengine wawili (02) wanaendelea na taratibu.

## Ufanisi wa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

Mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari umeimarisha usalama barabarani, Mfumo huu umeboresha uchunguzi wa ajali na kurahisisha usimamizi wa ratiba za madereva.

Jumla ya magari 11,826 yameunganishwa kwenye mfumo kati ya hayo, magari 8,969 yanatuma taarifa kwenye mfumo mpaka sasa na wastani wa magari 5,800 yanafanya safari kila siku katika nchi yetu. Aidha, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) umewezesha utambuzi wa madereva aliyethibitishwa, wakati akiwa barabarani.

## Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App)

LATRA imeandaa mfumo tumizi unaopatikana kwenye simujanja 'Play Store' za aina ya Android.

Huduma hii inamwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi, kutambua uhalali wa leseni za magari na adhabu, hivyo kumuwezesha abiria kuepuka kutumia gari lenye changamoto ili kujiepusha na usumbufu.



## Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho

LATRA inatumia Mfumo wa Serikali wa e-Mrejesho unaotumika kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo. Mfumo unapatikana kwa anwani ya https://emrejesho.gov.go.tz/ au kwa kupakua mfumo tumizi wa eMrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya LATRA www.latra.go.tz sehemu ya tovuti mashuhuri. Hivyo, tunawasihi wananchi wote kutumia mfumo huo na tunawahakikishia kushughulikia masuala yatakayowasilishwa ndani ya siku 21 tangu utakapowasilisha lalamiko au maulizo yako.

## Huduma kwa Wateja

LATRA imeanzisha kituo cha huduma kwa wateja mwaka 2023/24 kinachofanya kazi kwa saa zote ili kurahisisha utatuzi wa migogoro na changamoto kwa wakati. Huduma za kituo hicho zinapatikana kupitia namba za kupiga bila malipo 0800110019 na 0800110020. Vilevile Mamlaka imeendelea kuzitangaza namba hizi kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii na kuzibandika katika maeneo mbalimbali yanayofikiwa na wadau wetu. Kwa sasa, namba hizi zinaandikwa kwenye milango ya mabasi ya mijini sambamba na viwango vya nauli. Tathimini ya wateja ya mwaka 2023/2024 inaonesha asilimia 82 ya wateja wanaridhika na huduma za msingi za LATRA

## Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport Regulation)

Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa (2021/2022 hadi 2025/2026) imeelekeza maboresho katika huduma za utalii nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, LATRA imefanya utambuzi wa mahitaji, utayari wa wadau, na maeneo ya uwekezaji nchini. Tathmini ya awali ya LATRA imebainisha maeneo yenye vivutio yaliyopo kwenye mikoa






nane (08) ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, na Mbeya.

Aidha, rasimu ya Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya zilishaandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikisha wadau. Kanuni hizo zilijadiliwa kwenye kikao cha Wadau kilichofanyika tarehe 23 Disemba 2024. Pia, Bodi ya LATRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inakamilisha mapitio ya Muundo wa Uongozi na Mgawanyo wa Majukumu ili kuunda Kitengo cha Udhibiti Usafiri wa Waya na kuwezesha usimamizi wa Kanuni za Usafiri wa waya, pindi zitakapokamilika na kuidhinishwa na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwa mujibu wa Kanuni ya 45 ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

## Huduma za Usafiri wa Reli

Usafirishaji kwa njia ya reli nchini ni mojawapo ya eneo linalodhibitiwa na LATRA kwenye maeneo ya usalama wa miundombinu na mabehewa, nauli, viwango vya ubora na ufanisi wa utendaji. Katika hatua ya kutimiza majukumu haya, LATRA katika kipindi kinachoanzia Februari, 2021 hadi Machi, 2025 imefanya jumla ya kaguzi 275 katika miundombinu, ishara na mawasiliano, vitembea reli (vichwa na mabehewa) na uendeshaji. Kati ya kaguzi hizi, 143 zilikuwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), na kaguzi 132 zilikuwa kwa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

## Uanzishwaji wa Huduma za Treni za SGR

Katika maandalizi ya kuanza kwa huduma za usafiri wa abiria kwa treni za SGR, LATRA ilikuwa na jukumu la kuthibitisha ubora wa vitembea reli kabla ya kuanza kutoa huduma. LATRA iliungana na timu ya wataalamu wa TRC na Wizara ya Uchukuzi kwenda Nje ya Nchi (zilikokuwa zinaundwa) na kukagua na kuthibitisha. Jumla ya vichwa vya treni 17, Mabehewa ya abiria 56, treni za seti za umeme (EMU) 10 na Mabehewa ya mizigo 264 yamekaguliwa kipindi cha uundwaji katika nchi za Korea, China, Malaysia na Ujerumani. Mamlaka imefanya kaguzi za majaribio kwa mabehewa na vichwa hivyo baada ya kuwasili nchini kabla ya kuanza kutumika kutoa huduma.



**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), likiongozwa na Bodi ya Wahariri**

**Mwenyekiti:** CPA HABIBU JUMA SULUO | **Mhariri Mkuu:** SAMUEL KEENJA | **Wahariri Wasaidizi:** SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE| **Waandishi:** MAMBWANA JUMBE, NANCY AMANI na MARYAM NINA | **Msanifu Jarida:** IBRAHIM SAID